# COUNTY HIGH SCHOOL

**PANELI LA KISWAHILI**

**COMPILED BY:**

**BURALE & FEISAL SHAKIR**

**Gafkosoft.com/swa**

# Isimu Jamii

Isimu Jamii (social linguistcs) - ni tawi la isimu (elimu ya lugha) linalochunguza namna lugha inavyotumika katika jamii na uhusiano baina yake. Tawi hili huzingatia matumizi ya lugha katika mazingira tofauti; aina mbali mbali za lugha na mazingira yake; uhusiano kati ya lugha na utamaduni wa jamii inayoitumia.


- Istilahi za Isimu Jamii
- Aina za Lugha


## Istilahi za Isimu Jamii

1. **Isimu (linguistics)** - ni mtalaa ambao huchunguza, huchanganua na pia kuchambua na kufafanua lugha kama mfumo wa mawasiliano baina ya wanadamu.
2. **Lugha** - ni chombo cha mawasiliano baina ya watu. Lugha huzingatia mpangilio maalum wa sauti, maneno na sentensi.
3. **Sajili** - ni mukhtadha/rejista mbalimbali au mitindo maalum ya lugha katika mazingira/hali mbalimbali. Mifano ya sajili ni kama vile lugha ya hospitalini, shuleni, sajili ya dini, biashara, kisiasa, michezo,
4. **Fonolojia** - ni tawi la sayansi ya isimu linaloshughulikia uchunguzi wa **mfumo wa sauti** katika lugha fulani, kwa mfano ugawanyaji wa irabu na konsonanti. Fonolojia hutumika kuunda **alfabeti** katika lugha fulani. Aghalabu kila lugha hutumia mfumo fulani wa sauti mahususi katika lugha hiyo pekee.
5. **Fonetiki** - huchunguza sauti zinazotamkwa na binadamu bila kuzingatia lugha yoyote.
6. **Mofolojia** - (au sarufi maumbo) ni tawi la isimu linalochunguza maneno ya lugha fulani, aina za maneno katika lugha, hasa upangaji wa mofimu mbalimbali zitumikazo kwa ajili ya kuunda maneno hayo. Kwa mfano, lugha ya Kiswahili hutumia mbinu kadhaa kuunda maneno kulingana na mpangilio wa mofimu. Kwa mfano, neno 'lima' linaweza kutumika kuunda maneno mengine katika Kiswahili k.m mkulima, kilimo, nimelima, limika n.k Katika kubadilisha mofimu hizi, tunaweza kubadilisha neno moja kutoka aina moja(kitenzi) hadi nyingine (nomino) n.k
7. **Sintaksi** - (au sarufi miundo) ni tawi la isimu au taaluma ya sarufi inayoshughulikia jinsi vikundi vya maneno na sentensi mbalimbali zinajengwa katika lugha. Sintaksia huangazia kanuni au sheria za lugha. Kila lugha huwa na sheria zake za kuambatanisha maneno kama vile jinsi ya kufuatanisha vitenzi, nomino na vielezi. Kwa mfano: *Mtoto yako shiba* ni sentensi isiyokuwa na sintaksi. Sentensi sawa ingekuwa: *Mtoto wako ameshiba*.
8. **Semantiki** - ni tawi la isimu linalochunguza maana halisia (**mantiki**) ya maneno, kifungu au sentensi katika lugha.

Sentensi isiyokuwa na mantiki ni sentensi inayotoa maana ambayo haiwezekani katika uhalisia. Sentensi inaweza kuwa sawa kisintaksia lakini iwe na makosa ya kimantiki. Kwa mfano: *Kiatu cha mbwa kimefutwa kazi kwa sababu kumi ni kubwa kama hewa.*

## Aina za Lugha Katika Isimu Jamii

1. **Lafudhi** - Ni upekee wa mtu katika matamshi (accent) unaoathiriwa na lugha ya mama, mazingira yake ya kijiografia au kiwango ujuzi wake wa lugha.
2. **Lahaja** - ni vijilugha vinavyoibuka kwa lugha moja kuu kutokana na tofauti za kijiografia baina ya wazungumzaji wa lugha hiyo. Kwa mfano lugha ya Kiswahili ina lahaja kadhaa kama vile Kimtang'ata, Kilamu, Kimvita, n.k. Tofauti baina ya lufudhi ni kama msamiati, muundo wa sentensi au matamshi.
3. **Lugha rasmi** - ni lugha inayotumika katika shughuli za kiofisi ama ya wakati wa mawasiliano rasmi katika taifa fulani. Kwa mfano, lugha rasmi nchini Kenya ni Kiingereza.
4. **Lugha rasimi** - ni mtindo wa lugha uliotumiwa na mtu/watu fulani mashuhuri (zamani) na ambao huonekana kuwa mtindo bora wa lugha unaofaa kuigwa na wengine. Kwa mfano lugha ya Shakespeare.
5. **Lugha ya taifa** - ni lugha inayoteuliwa na taifa fulani kama chombo cha mawasiliano baina ya wananchi, kwa maana inazungumzwa na wananchi wengi katika taifa hilo. Lugha ya taifa, nchini Kenya ni Kiswahili; Uganda ni Kiganda.
6. **Lugha Sanifu** - Ni lugha iliyokarabatiwa na sheria zake (k.v muundo wa sentensi, msamiati, sarufi, n.k) kubainishwa na kuandikwa, na kwa hivyo huzingatia sarufi maalum na upatanisho sahihi wa sentensi. Kwa mfano: Kiswahili sanifu - ni lugha isiyokuwa na makosa ya kisarufi.
7. **Lingua Franka** - Ni lugha inayoteuliwa miongoni watu wenye asili tofauti wasiozungumza lugha moja ili iwe lugha ya kuwaunganisha katika shughuli rasmi au za kibiashara.
8. **Pijini** - ni lugha inayozaliwa kutokana na mchanganyo wa lugha zaidi ya moja. Kwa mfano. Sheng' (lugha ya vijana mitaani nchini ni lugha iliyoibuka kutoka kwa Kiswahili na Kiingereza.
9. **Krioli** - Ni pijini iliyokomaa na kukubalika.
10. **Lugha mame** - hii ni lugha isiyokua na ambayo hubaki kati umbo lake la awali. Kwa mfano lugha ya Kilatini haibadiliki na hivyo hutumika katika kubuni majina ya kisayansi, n.k.
11. **Lugha azali** - ni lugha inayozaa lugha nyinginezo.
12. **Misimu** - ni lugha yenye maneno ya kisiri ambayo hutumiwa na kikundi fulani cha watu katika jamii, inayoeleweka tu baina yao. Misimu huibuka na kutoweka baada ya muda.

# Sajili Katika Isimu Jamii

---

**Sajili** - ni mukhtadha/rejista mbalimbali au mitindo maalum ya lugha katika mazingira/hali mbalimbali.

Kuna sajili anuwai za matumizi ya lugha katika jamii. Hapa tutazingatia mifano michache ya sajili mbali mbali.Kila sajili huwa na sifa mbalimbali zinazoitofautisha sajili hiyo na nyinginezo. Ili kubaini sifa za lugha katika sajili fulani, ni muhimu kuzingatia baadhi ya maswali yafuatayo:

- ni mazungumzo baina ya nani na nani?
- kuna uhusiano gani baina ya wanaozungumza?
- yanapatikana wapi?
- yanatumika katika hali gani?
- yana umuhimu ama lengo gani
- ni istilahi zipi istilahi (maneno maalum) zinazopatikana katika mazingira hayo?
- umaizi wa lugha baina ya wazungumzaji ni wa kiwango gani?
- ni mtindo gani wa lugha unaotumika?

# Sajili ya Matanga

---

Ni lugha inayotumiwa katika shughuli za mazishi au nyumbani kwa marehemu.

## Sifa za Lugha ya Matanga/Mazishi

1. Hutumia msamiati wa maneno ya huzuni kama vile waombolezaji, makiwa, kifo, mauti, pole n.k.
2. Hutumia lugha ya kuliwaza/kufariji na kupa matumaini hasa kwa waombolezaji.
3. Ni lugha yenye unyenyekevu isiyotumia maneno yanayokera.
4. Hudhihirisha unyonge wa mwanadamu, kama asiye na mamlaka juu ya uhai wake.
5. Huwa na mbinu rejeshi kurejelea maisha ya marehemu alipokuwa hai.
6. Kwa mara nyingi hutumia maneno ya kusifu marehemu kutokana na aliyotenda.
7. Wakati mwingine huwa ni lugha inayodhihiri hali ya kukata tamaa.

## Mfano wa Sajili ya Matangani

"Waombolezaji wenzangu, kama mnavyojua tumekusanyika hapa kwa ajili ya kumsindikiza rafiki yetu amabye amelala hapa. Ikiwa kuna mtu alifikwa zaidi na msiba huu ni mimi. Marehemu alikuwa rafiki wangu wa dhati tuliyeshirikiana naye sana. Nilimjua marehemu tukifanya kazi katika soko la Mauzoduni na tangu siku hiyo tumeishi kama ndugu; kuomba radhi ukikosewa; kusaidiana, na kadhalika. "

Habari za kifo chake zilinipiga kwa mughdha. Sikuamini kwamba amekufa; kwamba sitamwona tena aushini mwangu. Ninasikitika sana lakini kwa kuwa Mungu hakosi, ninaamini kwamba alimpenda zaidi ya tulivyompenda. Ombi langu kwa Mungu ni moja, kwamba amweke rafiki yangu mahali pema peponi; au popote alipojitafutia siku zake za uhai; nami nitakapokufa anipeleke papo hapo tuendelee kuwa marafiki. Mwenzangu lala. Lala salama tutaonana siku moja"

# Sajili ya Ajali

---

Hii ni lugha inayotumiwa katika ambalo ajali imetokea. Wahusika wanaweza kuwa majeruhi, polisi, walioshuhudia au wananchi wengine n.k

## Sifa za lugha inayopatikana katika sajili hii

1. Msamiati wa kipekee unaohusiana na ajali kama vile majeruhi, hudumanya kwanza, damu, mkasa.

2. Hutumia lugha ya kudadisi dadisi ili kubaini chanzo cha ajali.
3. Huwa na masimulizi – walio na habari kuhusu kisa hicho hueleza waliyoshuhudia
4. Kutokana na hali ya msukosuko, lugha hii haina utaratibu – watu huwa katika hali ya hofu, kwa juhudi za kuwaokoa majeruhi.

## Mfano wa Sajili ya Ajali

| | |
|---|---|
| Mwanakijiji 1: | Nimesikia twa! Kisha kishindo kikubwa sana (akihema hema) Nikaambia kuna mlipuko tukimbie. |
| Mwanakijiji 2: | Lilio la muhimu ni kuyaokoa maisha ya majeruhi kwa kuwapa huduma ya kwanza. |
| Mwanakijiji 1: | Tuondoeni miili ya waliofariki kwanza. |
| Mwanakijiji 2: | hatuwezi kuishika miili iliyobanwa katika gari hadi polisi wafike. Na ndio hao wanaokuja! |
| Mwanakijiji 1: | (akikimbia) Ndio hao! Acheni kuiba mafuta! Polisi wanakuja! |
| Polisi: | Wakitawanya wananchi walioliparamia gari kuiba bidhaa mbali mbali.Liinueni hili gari! Wapi dereva? |
| Dereva: | (ambaye amelala akihema kwa maumivu, damu ikichuruzika miguuni na mikononi) Nilisitishwa na ng'ombe waliokuwa wakivuka barabara. Nilijsribu kukwepa lakini usukani ukanishinda gari likapoteza mwelekeo… |
| Abiria: | Alikuwa akiendesha gari kwa kasi sana. Tukampigia kelele apunguze mwendo lakini hakutusikia. Matunda yake… |
| Mwanakijiji 2: | Niliona gari likibingiria mara kadhaa mpaka likaingia humu mtaroni, ndiyo tukakimbia kuwaokoa. |
| Polisi: | Nyamazeni! Achieni polisi kazi iliyobaki. Ikiwa kuna yeyote anayejuana na waathiriwa aandamane nasi. |

# Sajili ya Nyumbani

Hii ni lugha inayotumiwa na watu katika familia. Wanaohusika sana katika mazungumzo ya nyumbani ni mama, baba, watoto, majirani na watu wa ukoo. Maswala yanayorejelewa sana ni yale yanayoiathiri jamii/boma hilo.

## Sifa za Sajili ya Nyumbani

Sifa za sajili ya nyumbani hubadilika kulingana na mada inayorejelewa, wanaozungumza na hali katika boma.

## Mfano wa Sajili ya Nyumbani

| | |
|---|---|
| Baba: | Mama Kadara! Huyo mtoto wako amekuja? |
| Mama: | Kadara ni mtoto wetu; mimi na wewe. |
| Baba: | Hapana! Mimi sizai malaya. Huyo ni wako. Hata Bahati ni wako! Hakika wote sita ni wako… |
| Mama: | Mume wangu unanifanya nikasirike bure tu. Mbona umeanza mafarakano tena. |
| Baba: | Mafarakano! Mafarakano! Ni mimi niliyekwambia uzae wasichana sita… |
| Mama: | Lakini sikuzaa pekee. Tulizaa na wewe, mume wangu…. |
| Baba: | Hapana! Uliniona na mimba? Uliniona na maumivu ya uzazi? Umeniona nikinyonyesha mtoto? Mwanamke kuwa na adabu. Nitakurudisha kwa wazazi wakufunze heshima. Na nitaoa sioni tukikaa pamoja. |
| Mama: | (baada ya kimya) Niambie ulichotaka kuniambia kuhusu Kadara (akijipangusa machozi kwa kitambaa) unajua |

| | |
|---|---|
| | mume wangu, nakuheshimu. Yangalikuwa mapenzi yangu tungepata wavulana pia. Lakini haya ni mapenzi ya Mungu. |
| Baba: | Kadara akija umpe kuku apeleke vileoni kwa Mzee Magoti. Nina deni lake kubwa baada ya kunywa tembo siku kadhaa bila kulipa. (akicheka) Hakika hata anastahili mbuzi. |
| Mama: | Hatuwezi kulipia pombe kwa mbuzi wala kuku. Kuku waliobaki hapa ni wangu na wa watoto wangu. Kuku wako uliwauza. |
| Baba: | Kelele za chura hazimkatazi ng'ombe kunywa maji. Endelea kupayuka kama wanawake wengine wa kijijini. Nikirudi nikute chakula na maji moto tayari. |
| Mama: | (akinuna) Haya nimesikia. |

# Sajili ya Simu

Hii ni lugha inayotumiwa katika mazungumzo ya simu.

## Sifa za lugha ya simu

1. Mazungumzo ya simu ni mafupi, hutumia sentensi fupi zenye muundo rahisi.
2. Hoja hutajwa moja kwa moja bila maneno mengi kwani ili kudhibiti gharama ya simu
3. Huwa na kukatizana kwa maneno kati ya wazugumzaji.
4. Huwa ni mazungumzo baina ya watu wawili pekee; anayepiga na anayepokea.
5. Hutumia istilahi maalum za lugha ya simu kama neno 'hello'
6. Huchanganya ndimi (kutumia maneno yasiyo ya lugha nyinginezo) ili kuwasilisha ujumbe kwa upesi.
7. Ni lugha ya kujibizana.

## Mfano wa Sajili ya Simu

| | |
|---|---|
| Sera: | Hello. Ningependa kuongea na Mika. |
| Sauti: | Subiri kidogo nimpatie simu. |
| Sera: | Hello |
| Mika: | Hello. Sema Sera. Niko kwa mkutano… |
| Sera: | Pole kwa kukusumbua. Unakumbuka safari yetu ya kesho? |
| Mika: | Siwezi kusahau. Tunakutana saa ngapi? |
| Sera: | nampendekeza saa tano machana… |
| Mika: | Katika Hoteli ya Katata Maa |
| Sera: | enhe. Hapo kwa heri |
| Mika: | Haya. Bye! |

# Sajili ya Biashara

Lugha ya biashara huzungumzwa na wauzaji na wanunuzi katika sehemu za kibiashara. Inapaswa ikumbukwe kwamba lugha hii inaweza kubadilika kidogo kulingana na mazingira. Kwa mfano, katika mikutano ya kibiashara, lugha rasmi hutumiwa ilihali katika soko, lugha ya mitaani inaweza kutumika.

## Sifa za Lugha ya Biashara

1. Hutumia msamiati wa kibiashara kama vile:
   - Fedha
   - Faida
   - Hasara
   - Bei
   - Bidhaa
2. Hutumia misimu ili kuwavutia wanunuzi

3. Ni lugha yenye malumbano hasa watu wanapojadiliana kuhusu bei
4. Ni lugha legevu - haizingatii kanuni za lugha.
5. Huchanganya ndimi kwa kuingiza maneno ya lugha za kigeni
6. Ni yenye heshima na unyenyekevu kwa wanunuaji
7. Msamiati katika lugha ya Kibiashara

## Mfano wa Sajili ya Biashara

| | |
|---|---|
| Mtu X: | Tatu kwa mia! Tatu kwa mia! Leo ni bei ya hasara! |
| Mtu Y: | Unauza hii briefcase kwa pesa ngapi? |
| Mtu X: | Hiyo ni seventy bob mtu wangu |
| Mtu Y: | Huwezi kunipunguzia. Niuzie hamsini hivi. |
| Mtu X: | Haiwezekani mtu wangu. NItapata hasara nikiuza hivyo. Ongeza mkwaja, mama. |
| Mtu Y: | Basi hamsini na tano. |
| Mtu X: | Tafadhali ongeza kitu kidogo. Unataka nikule hasara leo? Fikisha sitini na tano. |
| Mtu Y: | Basi sitanunua hii. Sina pesa hizo zote. Unajua uchumi ni mbaya siku hizi. |
| Mtu X: | Tafadhali mtu wangu. Huu mkoba ni mzuri sana. Umetoka Germany. Angalia. Unaweka pesa hapa, kitambulisho hapa halafu unafunga hivi. Hauwezi kupoteza chochote ukiwa na mkoba huu. Angalia wewe mwenyewe. Hakuna mahali pengine utaweza kununua mkoba huu kwa bei ghali kama hii. |
| Mtu Y: | Nimekwambia sina hizo pesa. Nitanunua baadaye ukipunguza bei. |
| Mtu X: | Lete sixty bob. Lakini utakuwa umeniumiza. Nakufanyia hivyo kwa kuwa wewe ni customer poa. |
| Mtu Y: | Sawa basi nitanunua. Shika sixty bob. |
| Mtu X: | Asante Customer. Mungu akubariki. (akimfungia) Hey! Tatu kwa mia. Bei ya hasara! Tatu kwa mia! |

# Sajili ya Bungeni

---

Hii ni lugha inayozungumzwa wakati wa kikao cha bunge. Sajili hii ni tofauti na na sajili ya siasa, ambayo huhusisha wanasiasa wakipiga kampeni.

## Sifa za Lugha ya Bungeni

1. Ni lugha yenye ushawishi – wabunge hutumia vishawishi ili kuwahimiza wenzao waunge ama kupinga msalaba
2. Ni lugha ya mjadala yenye waungao na wapingao.
3. Ni lugha yenye heshima na nidhamu. Maneno ya heshima kama mheshimiwa, tafadhali na samahani hutumika sana.
4. Hutumia maneno maalum yanayopatikana katika mazingira ya bunge kama vile kikao, mswaada, kuunga mkono, kujadili, kupitisha, n.k.
5. Lugha ya bungeni ni rasmi na sanifu.
6. Hulenga maswala mbalimbali ya kisiasa na maendeleo katika taifa.
7. Huwa na maelezo kamilifu
8. Ni lugha yenye maswali na majibu miongoni mwa wabunge.

## Mfano wa sajili ya Bungeni

| | |
|---|---|
| Spika: | Waheshimiwa, muda unayoyoma. Nawaomba mfanye mazungumzo yenu sauti ya chini tumsikize huyu. |

| | |
|---|---|
| | Endelea mheshimiwa. |
| Mbunge 1: | Asante Bwana spika. Hii siyo mara ya kwanza ya kuuwasilisha mswaada huu hapa. Kila mbunge anayethamini raia wa taifa hili ni lazima auunge mkono mswada huu. Katika kikao kilichotangulia, mliupinga mkidai kwamba hauna heshima kwa rais. Leo tumefanya ukarabati wote mliotaka. Hamna budi kuuunga mkono. Bwana spika…. |
| Spika: | Muda wako umekwisha tafadhali keti. Wabunge wataamua hatima ya mswada huu ikiwa utapitishwa kama sheria. Lakini kumbukeni uamuzi wa mwisho ni wa rais. |

# Sajili ya Hospitalini

---

## Sifa za Lugha ya Hospitalini

1. Hutumia msamiati wa hospitalini kama vile
    - dawa
    - magonjwa
    - Daktari
    - Wadi
    - Mgonjwa
    - Dawa
    - Kipimo
2. Ni lugha yenye upole na heshima
3. Huwa na maswali mengi hasa daktari anapotaka kutambua kiini cha ugonjwa unaomhadhiri mgonjwa wake
4. Ni lugha yenye hofu na huzuni

## Mfano wa Sajili ya Hospitalini

| | |
|---|---|
| Daktari: | Ulianza kuumwa hivi lini? |
| Mgonjwa: | Kichwa kilianza kuniuma jana jioni baada ya chajio. Nilipoamka asubuhi nikatambua kwamba hata tumbo lilikuwa likiuma pia. |
| Daktari: | Ulipoanza kuumwa na mwili mzima, ulichukua hatua gani? Hukunywa dawa yoyote? |
| Mgonjwa: | Nilichukua tembe zilizokuwa zimepatiwa kakangu miaka mitano iliyopita alipokuwa akiumwa na malaria. |
| Daktari: | Kila ugonjwa unahitaji matibabu mbalimbali. Tembe za malaria haziwezi kutumika kutibu maumivu ya kichwa na tumbo. Pia ni hatari kutumia dawa ambazo zimepitwa na wakati. Zinaweza kukuletea madhara zaidi. |
| Mgonjwa: | (akikohoa) Sijui kama una tembe za kifua pia. Hii baridi inaniletea homa mbaya. |
| Daktari: | Hatuwezi kukupatia dawa kabla ya kutambua ugonjwa ulio nao. Itabidi tupime joto lako, damu na pia mate yako ili kupata tatizo linalokusumbua. Kisha tutakupatia dawa. Je, una umri wa miaka mingapi? |
| Mgonjwa: | Nikichukua hizo dawa nitapona? |
| Daktari: | Matokeo hubadilika kutoka kwa mgonjwa mmoja hadi mwengine. Inaweza kuchukua muda. Huenda ukalazwa kwenye wadi kwa siku mbili tatu hivi. Umri wako, mama? |

# Sajili ya Kidini

---

Katika sajili ya kidini tunaangazia lugha inayozungumzwa na waumini/washiriki wa imani fulani wakati wa ibada, sala, katika nyumba takatifu au mahali popote pale ambapo wanazungumzia mambo yanayorejelea imani au Mwenyezi Mungu.

## Sifa za Lugha ya Kidini

1. Hutumia msamiati wa kidini kama vile
   - Bibilia
   - maombi
   - mbinguni
   - jehanamu
   - Madhabahu
   - Paradiso
   - Mbinguni
   - Mwenyezi Mungu
   - Mwokozi
2. Ni lugha inayonukuu sana hasa wazungumzaji wanaporejelea Kitabu kitakatifu
3. Lugha yenye heshima, upole na unyenyekevu
4. Lugha sanifu
5. Ni lugha iliyojaa ahadi nyingi kwa wanaoandamana na mafunzo ya kidini na vitisho kwa wanaoenda kinyume na mafundisho
6. Huwa imejaa matumaini
7. Ni lugha yenye kutoa maneno ya sifa, kumtukuza na kumshukuru Mwenyezi Mungu

## Mfano wa Sajili ya Kidini

| | |
|---|---|
| Boriti: | Bwana asifiwe Bi... |
| Bi Rangile: | Amina, mchungaji. Watoto wanaendeleaje? |
| Boriti: | Karita hana neno. Mwenyezi Mungu ametunyeshea rehema na neema zake. Je, wajukuu wako wa hali gani? |
| Bi Rangile: | Wanaendelea vizuri isipokuwa hawataendelea na masomo. Sijui nilimfanyia Mungu dhambi gani. |
| Boriti: | Nasikitika sana kusikia hivyo. Mungu atawalinda mayatima hao. Yeye ndiye baba wa mayatima. Mungu ni mwenye huruma. |
| Bi Rangile: | Sijui hayo, mchungaji. Hata sijui maana ya kuishi hapa duniani. Kila siku ni matatizo. |
| Boriti: | Usife moyo. Mungu anasema katika kitabu cha Yohana 14:18, "Sitawaacha nyinyi kama mayatima..." Kwa hivyo, ukiwa na imani, Mungu atakuonekania. |
| Bi Rangile: | Basi niombee mchungaji ili Saumu na Neema wapate karo ya kurudi shuleni. |
| Boriti: | Funga macho tusali. Ewe Rabuka uliyejaa neema na baraka tele. Tunakushukuru na kulitukuza Jina lako takatifu kwa baraka zako za ajabu. Tunajua kwamba wewe ndiye Mungu uliyewatoa wana wa Israeli kutoka Misri. Sisi wenye dhambi tunakuja mbele yako tukiomba ukafanya miujiza katika nyumba hii ya Bi Rangile...... |
| Wote: | Amina. |

# Sajili ya Mahakamani

---

Hii ni lugha inayozungumzwa na wanasheria, mahakimu, mawakili, washitakiwa na mashahidi katika mahakama.

## Sifa za Lugha ya Mahakamani

1. Hutumia msamiati wa kipekee unaorejelea sheria kama vile
   - katiba
   - sheria
   - mashtaka
   - Hakimu
   - Ushahidi
   - Wakili
   - Jela
   - Mshitakiwa

- Kiongozi wa mashtakiwa

2. Huwa na maelezo marefu na ya kina ili kutafuta ushahidi wowote uliopo
3. Ni lugha yenye kunukuu sana hasa vipengele katika vitabu vya sheria kama vile katiba
4. Ni lugha rasmi na sanifu
5. Ni lugha iliyojaa maswali na majibizano
6. Ni lugha yenye heshima

## Mfano wa Sajili ya Mahakamani

| | |
|---|---|
| Kiongozi: | Musa Kasorogani, mwanaye Bi Safina na Mzee Mpotevu Kasorogani; umeshtakiwa kwa kosa la jaribio la mauaji mnamo tarehe 23/08 mwaka huu. Unaweza kukubali mashitaka, kukana au kunyamaza. Je, unakubali mashitaka. |
| Musa: | Naomba kukanusha mashtaka hayo, bwana mkubwa. |
| Kiongozi: | Je, kuna shahidi yeyote katika kesi hii? |
| Katili: | Hapa mkubwa. Siku hiyo ya tarehe 23/08, Musa alipatikana akiwa akijinyonga usiku wa maneno. Kijiji chote kilikusanyika hapo kwenye boma ya Kasorogani. Nilipoleta polisi, wakamkamata na kumpeleka hospitalini atibiwe kwanza. Ndiposa ameletwa hapa siku ya leo. |
| Kiongozi: | Je, mshitakiwa una tetesi lolote. Ama pia unaweza kuleta wakili wako azungumze kwa niaba yako. |
| Kisaka: | Bwana mkubwa, mimi ndiye wakili na shahidi wa Musa. Musa hakuua mtu. Alikuwa akijinyonga kutokana na mkasa uliomfika tarehe hiyo ya Agosti 23 baada ya bibi harusi wake kubadilika. Mimi na mamake, Bi Safina Kasorogani tulijaribu kumtuliza jioni hiyo. Asubuhi nilipoamka siku iliyofuatia, nikapata habari kwamba alikuwa amepelekwa hospitalini. Je, alipojaribu kujiua, alimwua mtu yeyote? |
| Kiongozi: | Kulingana na katiba ya nchi hii, kifungu cha 12.ab, kuua ni kutoa uhai wa binadamu yeyote. Haijalishi ikiwa ni yeye mwenyewe au ikiwa ni rafiki yake. Hivyo basi jaribio la kujiua ni hatia kulingana na kanuni za nchi hii. Una jingine la kuulizia? |
| Kisaka: | Je, sheria yetu inaruhusu mtu kuadhibiwa kwa kosa ambalo hakufanya? |
| Kiongozi: | La hasha. |
| Kisaka: | Basi tutakuwa tumekiuka kanuni za nchi yetu iwapo tutamhukumu Musa kwa kujiua ilhali hakujiua bado. Tunawezaje kutambua kama angekufa? |
| Katili: | Inafaa ahukumiwe kinyonga au kifungo cha maisha gerezani. Hata alivunja simu yangu... |
| Kiongozi: | Order! Lazima kutii mpangilio wa mahakama. Katili hauruhusiwi kuongea bila ruhusa ya hakimu au kiongozi wa mashitaka. Polisi, mpelekeni nje. |

# Sajili ya Michezoni

---

Lugha ya michezoni hutumiwa wakati wa mashindano ya michezo kama vile kandanda, ukimbiaji n.k Hii inaweza kuwa lugha ya watangazaji/wasimulizi wa mchezo, watazamaji, mashabiki au wachezaji.

## Sifa za Lugha ya Michezoni

1. Hutumia msamiati wa kipekee unaohusu michezo kama vile mpira, goli, mchezaji
2. Huchanganya ndimi na kuingiza maneno ya lugha nyingine kama vile Kiingereza. mfano 'goal!!!'
3. Ni lugha ambayo hutumia vihisishi na mshangao kwa wingi
4. Sentensi nyingi katika lugha hii huachwa bila kukamilika hasa hali inapobadilika uwanjani

5. Husimuliwa kwa haraka haraka ili kuambatana na kasi ya mchezo
6. Ni lugha yenye sifa na na chuku kwa mfano msimulizi anaposimulia sifa za mchezaji fulani
7. Hutumia misimu kama vile 'wametoka sare'
8. Hutumia kwa ya kulinganisha ili kuelezea matokeo ya mechi k.m 'walitoka mbili kwa nunge'
9. Ni lugha yenye kukariri (kurudia rudia) hasa mchezaji anapoumiliki mpira kwa muda mrefu au mwanariadha fulani anapoelekea kushinda katika mbio.
10. Huwa na sentensi fupi fupi

## Mfano wa Sajili ya Michezoni

Nakwambia ndugu msikilizaji hapa mambo yamechacha kwelikweli. Hawa wachezaji wa Manyuu hawacheki na watu leo. Wameamua kuishambulia timu ya Cheusi bila huruma. Kumbuka kwamba hii ni mara yao ya... Lo! Anauchukua mpira pale, mchezaji nambari tisa... Matiksta. Matiksta, Matiksta na mpira. Anaucharazacharaza pale. Anamwangalia mwenzake. Anaupiga mpira kwa kichwa pale! Lo! Mwenzake anaukosa. Akiushika mpira pale ni mchezaji wa timu ya Cheusi, Romana. Romana, Romana anaelekeza mpira kwenye lango la Manyuu. Anaupiga mpira kwa nguvu! Lo! Hatari sana. Hatari sana katika lango la Manyuu. Hatari! hatari! Gooooaaaaaal! Noooo ooh! Wameukosa! Goal keeper ameudaka mpira huo. Pole sana wachezaji wa ... Mlinda lango anaupiga mpira huo kwa hasira. Juu kabisa. Anauchukua pale nambari saba, Saruta. Huyu ni mchezaji machahari sana. Mwaka uliopita, alipewa tuzo la mchezaji bora wa mwaka. Ananyang'anywa na mchezaji mwingine hapa. Wanakabiliana kidogo. Huyu mchezaji anaupiga mpira kwa mguu wa kushoto. Lo! Mpira umekuwa mwingi na ukatoka nje.

Mashabiki wa timu hizi mbili wanasubiri kwa hamu na ghamu kutambua ni nani atakayeibuka mshindi. Katika mechi zilizotangulia, timu hizi zimekuwa zikitoka sare. Lakini leo lazima mshindi atapatikana. Hawa ni fahali wawili. Kumbuka kwamba unapata matangazo haya moja kwa moja kupitia idhaa yako uipendayo, redio nambari moja kote nchini... Mpira unarudishwa uwanjani. Akienda kuurusha pale ni...

# Sajili ya Mtaani

---

Lugha ya mitaani ni lugha inayozungumzwa na vijana mtaani.

## Sifa za Lugha ya Mtaani

1. Ni lugha legevu isiyozingatia kanuni za kisarufi
2. Huchanganya ndimi
3. Hutumia misimu kwa wingi
4. Hukosa mada maalum

## Mfano wa Sajili ya Mtaani

| | |
|---|---|
| Chali: | Hey, niaje msupaa? |
| Katosha: | Poa. So, mathee yako alikushow naweza kuja? |
| Chali: | Ha! Masa hana noma. Si unajua nita... |
| Katosha: | Chali! Unataka aniletee problem? |
| Chali: | Mimi ni boy wa maplans. Ngoja nifikirie venye tutamshow |
| Katosha: | Na by the way, kwani umejipaka mafuta ya manzi. Ama ulikuwa na msichana mgani? |
| Chali: | Oh! Niliscoop mafuta ya Anita. Si unajua nataka |

| | |
|---|---|
| | kunukia hmmmm... |
| Katosha: | Ok. So, umefikiria tumshow nini masa yako? Ama nikona idea poa. |
| Chali: | Nishow hiyo plot, na by the way, nataka unisaidie kuhusu ile deal yangu na Kaunda. Ile ya siz yangu. |
| Katosha: | Kwanza tutaplan na huyo siz yako, niwe ndiye nimekuja kuvisit. Mamako atakubali |
| Chali: | Wow! Idea poa. Utakuwa umekuja kufanya homework. Halafu masa akiishia kwa bed. Homework tutaitupa mbali. |
| Katosha: | So, utamshow Anita nakuja tufanye homework... |

# Sajili ya Kisayansi

## Sifa za Lugha ya Kisayansi

1. Hutumia msamiati wa kipekee unaoambatana na taaluma inayorejelewa.
2. Huwa na maelezo kwa ukamilifu.
3. Huwa na mpangilio maalum na maendelezo ya hoja na ujumbe.
4. Huchanganya ndimi na kutumia maneno ya kisayansi au lugha mbalimbali.
5. Hutumia lugha sanifu.
6. Ni lugha yenye udadisi mwingi (wakati wa kufanya utafiti)

## Mfano wa Lugha ya Kisayansi

Kwa sababu zisizoweza kuepukika, kikundi chetu hakitamaliza utafiti ulioratibiwa kukamilishwa mwishoni mwa mwezi ujao. Hii ni kwa sababu ya changamoto kadhaa ambazo tumekutana nazo.

Kwanza, viluwiluwi, ambao ndio tunaotafiti wamekuwa haba sana wakati huu wa ukame. Pili, kutokana na kufungwa kwa maabara ya kisayansi katika taasisi hii, ni muhali kufanya majaribio yoyote ya kazi yetu. Tatu, kumekuwa na pingamizi kubwa kutoka kwa baadhi ya wanakijiji kwamba kukusanya viluwiluwi kunawatia hofu. Aidha, tume yetu imepungukiwa na fedha baada ya serikali kusitisha kudhamini utafiti huu.

Baada ya kujadiliana kwa vikao tatu mfululizo, tume yetu inapendekeza haya: Muda wa kufanya utafiti uongezewe kwa kipindi cha miezi sita; serikali kupitia kwa taasisi hii ifadhili wachunguzi. Wananchi wahamasishwe kuhusu umuhimu wa kuwafanyia viwavi utafiti na maabara ya utafiti ikaraatiwe haraka iwezekanayo.

# Sajili ya Shuleni

Hii ni rejista ya lugha inayopatikana katika mazingira ya shule. Wahusika wake huwa walimu, wazazi na wanafunzi.

## Sifa za Sajili ya Shuleni

1. Matumizi ya istilahi (maneno maalum) yanayopatikana katika mazingira ya shule kama vile darasa, mitihani, vitabu, elimu, muhula, masomo
2. Lugha yenye heshima kutokana na utofauti baina ya mwanafunzi na mwalimu, mzazi na mwalimu;
3. Takriri - mbinu ya kurudiarudia maneno. Katika darasa mwalimu hurudia rudia maneno ili kusisitiza anachofunza
4. Ni lugha yenye maswali mengi na majibu. Mwalimu huuliza maswali wakati wa mafunzo. Wanafunzi pia huuliza maswali ili kujua/kupata ufafanuzi.
5. Hutumia lugha ya kukosoana na kurekebishana.

# Mfano wa Mazungumzo katika Sajili ya Shuleni

## a) Mazungumzo kati ya Mzazi na Mwalimu

| | |
|---|---|
| Mwalimu: | Mzee Kundu, ningetaka tuzungumze kwa muda kuhusu hali ya mwanao, Machome Kundu. |
| Mzee: | Machome? Ana nini mwanangu. Kuna nafasi imepatikana ya… |
| Mwalimu: | Mwanako amebadilika sana kitabia. Alikuwa akifanya vizuri sana katika masomo |
| Mzee: | Kweli kabisa. Mimi ni mlezi mwema sizai watoto mbu mbu mbu darasani. |
| Mwalimu: | Ndivyo. Lakini sasa naona ameanza kubadilika. Ameanza kulegea katika mitihani na kuzembea kazini. |
| Mzee: | Unamaanisha nini? (akiinuka) Inaonekana siku hizi hamjui kuwapa adabu watoto. Ni lazima mtoto wangu amepotoshwa na wengine, katika vikundi vibaya! |
| Mwalimu: | Hakika, mwanako ndiye anayepotosha wanafunzi wengine. Yeye ni kiongozi wa makundi haramu shuleni, yanayovuruga masomo, kuuza dawa za kulevya na mambo kama haya. Hii ndiyo sababu nimekuita tujadiliane. Ni lazima mienendo hii imechipuka nyumbani. |
| Mzee: | Ajapo nyumbani, mwanangu huzingatia vitabu pekee hata mamake anaweza kuthibitisha haya. Ikiwa kuna utovu wa nidhamu nina hakika haya yanatoka darasani. |
| Mwalimu: | Tafadhali keti mzee (akichungulia dirishani) Mtindi! Niitie Machome… |

## b) Mazungumzo katika Sajili ya Darasani

| | |
|---|---|
| Mwalimu: | Toeni vitabu vyenu vya Historia mnakili haya. Ni nani atakayetukumbusha tulichosoma wiki jana? Naam Halima! |
| Halima: | Tulisoma kuhusu Chama cha Mapinduzi |
| Wanafunzi: | (Wakiinua mikono na kupiga kelele) Mwalimu Mwalimu |
| Mwalimu: | Inueni mikono nitawaona. Msipige kelele. Halima umenoa. Simama! Mwanafunzi mwengine? |
| Jadaha: | Tulisoma kuhusu kundi asi la Maji Moto lililopinga wakoloni. |
| Wanafunzi: | Mwalimu! Mwalimu! Kundi la Maji Maji. |
| Mwalimu: | Naam mmepata. Lakini nimewaambia msijibu kwa pamoja. Ukitaka kujibu uinue mikono. Jadaha, ni kundi la Maji Maji siyo Maji Moto. Leo tutasoma athari za kundi katika taifa letu la Tanzania na namna lilivyoshindwa nguvu. Lakini kabla hatujaendelea ningependa mniambie, ni matatizo yepi yaliyochochea kuchipuka kwa kundi hilo. |
| Kirata: | Mwalimu nina swali. Kiongozi wa kundi hilo alikuwa nani? |
| Mwalimu: | Kirata hukuwa darasani wiki jana. Nione baada ya kipindi hiki. (wanafunzi wakicheka) Nawe wafanyani na kitabu cha Hisabati katika somo la Historia. Kimbia ofisini unaletee kiboko. Ninyi ndio mnaorejesha nyuma darasa langu katika mitihani. |

# Fasihi Simulizi

---

| **FASIHI SIMULIZI** | |
|---|---|
| **Utanzu wa** | Fasihi |
| **Kiingereza** | Oral Literature |
| **Tanzu za Fasihi Simulizi** | • Hadithi / Ngano<br>• Nyimbo |

- Maigizo
- Tungo Fupi

---

**Prev** Tamathali za Usemi

**Next** Fasihi Andishi

**VIPERA VYA TANZU ZA FASIHI SIMULIZI**

| | |
|---|---|
| **HADITHI / NGANO** | • Khurafa<br>• Hekaya<br>• Mighani / Visakale<br>• Usuli / Visaviini<br>• Visasili<br>• Hadithi za Mtanziko<br>• Hadithi za Mazimwi |
| **NYIMBO** | • Mashairi<br>• Kimai<br>• Wawe/Hodiya<br>• Nyimbo za Ndoa<br>• Nyimbo za Kidini<br>• Nyimbo za Kisiasa<br>• Za Tohara/Jandoni<br>• Nyimbo za Kizalendo |
| **TUNGO FUPI** | • Methali<br>• Vitendawili<br>• Mafumbo<br>• Vitanza Ndimi na Vichezea Maneno<br>• Semi<br>• Lakabu<br>• Misimu |
| **MAIGIZO** | • Michezo ya Kuigiza<br>• Ngomezi<br>• Miviga<br>• Malumbano ya Utani<br>• Mazungumzo/Soga<br>• Ulumbi<br>• Vichekesho<br>• Maonyesho |

Fasihi Simulizi ni utanzu wa fasihi ambao unawakilisha sanaa ya lugha inayopitishwa kutoka kwa kizazi hadi kizazi kwa njia ya maneno/masimulizi ya mdomo.

## Sifa za Fasihi Simulizi

1. Hupitishwa kwa njia ya mdomo
2. Ufanisi wa sanaa katika fasihi simulizi hutegemea uwezo wa msimulizi, au wahusika
3. Masimulizi yake yanaweza kuathiriwa na mazingira, hisia na hali
4. Ni mali ya jamii. Hakuna mtu fulani anayemiliki sanaa katika fasihi simulizi.
5. Inaweza kubadilika kutoka kizazi hadi kizazi, au mazingira mbalimbali kwa sababu hutegemea kumbukumbu ya msimulizi.
6. Aghalabu huwa na funzo fulani

## Umuhimu wa Fasihi Simulizi

1. Kuburudisha - Hufurahisha na kuchangamsha hadhira
2. Kunasihi- kutolea mawaidha na kuonyesha mwelekeo unaotarajiwa katika jamii
3. Kuelimisha watu kuhusu vitu mbalimbali hasa mazingira yao
4. Kutambulisha jamii - jamii mbalimbali husifika kutokana na sanaa zao katika fasihi simulizi kama vile nyimbo
5. Kuhifadhi na kudumisha utamaduni wa jamii
6. Kuunganisha watu - huleta watu pamoja

7. Kukuza lugha - fasihi huimarisha lugha kwa kuwa hutumia mbinu mbalimbali za lugha.
8. Kuliwaza - hutoa huzuni na kuleta matumaini.
9. Kupitisha muda - wakati mwingine fasihi simulizi hutumika kupitisha muda.

---

# Ngano Katika Fasihi Simulizi

---

| HADITHI / NGANO | |
|---|---|
| **Utanzu wa** | Fasihi Simulizi |
| **Kiingereza** | Narratives |
| **Vipera vya Hadithi** | • Khurafa<br>• Hekaya<br>• Mighani / Visakale<br>• Usuli / Visaviini<br>• Visasili<br>• Ngano za Mazimwi<br>• Ngano za Mtanziko |

---

**Prev**

Hadithi (ngano) ni utungo wenye visa vya kubuni unaosimuliwa kwa lugha nathari kwa kusudi la kuburudisha, kukuza maadili na kuunganisha jamii. Msimulizi wa hadithi huitwa **Fanani** au **Mtambaji.**

**Content**


- Vipera vya Ngano
- Sifa za Ngano
- Umuhimu wa Ngano
- Sifa za Mtambaji wa Hadithi


## Vipera vya Ngano

Tunaweza kuainisha ngano kulingana na vipengele vifuatavyo:

1. Wahusika => k.v khurafa, hekaya, mighani, mazimwi,
2. Maudhui => k.v usuli, visasili, mtanziko

Utanzu huu wa fasihi simulizi umegawanyika katika vipera (aina) kadhaa:

| AINA | MAELEZO KWA UFUPI |
|---|---|
| Khurafa | hadithi ambazo wahusika ni wanyama. |
| Hekaya | mhusika mmoja (k.v sungura) huwa mjanja kuliko wenzake |
| Usuli (Visaviini) | huelezea chanzo cha jambo au hali fulani |
| Visasili | huelezea asili au chimbuko la jamii au mambo ya kiada k.v mauti, ndoa, tohara n.k. |
| Mighani (Visakale) | hadithi za mashujaa |
| Mazimwi | huwa na wahusika majitu au mazimwi |
| Mtanziko | humwacha mhusika katika hali ya kutojua chaguo linalofaa. Kila achagualo lina matukio mabaya. |

## Sifa za Ngano

1. Huwa na mianzo maalumu
    - Paukwa! Pakawa!
    - "Hadithi! Hadithi!" - "Hadithi Njoo!"
    - Hapo zamani za kale...
2. Huwa na miishio maalum
    - Hadithi yangu yaishia papo!
    - ...wakaishi kwa raha mustarehe.

3. Huwa na funzo fulani ambalo aghalabu hutajwa mwishoni mwa hadithi.
4. Masimulizi yake huwa kwa wakati uliopita
5. Husimuliwa kwa lugha ya natharia
6. Huwa na wahusika ambao wanaweza kuwa binadamu, wanyama, miungu, mashetani au vitu visivyo hai
7. Huhusisha mbinu nyingine za fasihi simulizi kama vile
    - Nyimbo - kuburudisha, kuamsha hadhira, kupitisha ujumbe
    - Methali - kutoa funzo
    - Misemo - kupamba lugha
    - Vitendawili na mafumbo - kushirikisha hadhira katika masimulizi
8. Hutumia mbinu ya takriri ili kusisitiza ujumbe kwa kurudiarudia maneno, matukio au nyimbo
9. Hutumia tamathali za lugha kama vile tashbihi, tashihisi, chuku, tanakali za sauti ili kupamba masimulizi n.k
10. Huwa na muundo rahisi wenye mwanzo, kati na mwisho.
11. Ufanisi wake hutegemea mbinu za mtambaji k.v ishara-uso na ubunifu wake jukwaani.
12. Sehemu fulani zinaweza kubadilishwa kulingana na hadhira

## Umuhimu wa Ngano

1. Kuhifadhi au kurithisha mali ya jamii
2. Kuunganisha na kukuza ushirikiano miongoni mwa jamii
3. Kuelemisha au kutoa mafunzo kuhusu mambo fulani
4. Kukuza maadili mema
5. Kuonya, kuelekeza, kuhimiza na kunasihi
6. Kuburudisha hadhira. Hadithi nyingi huwa na visa vya kusisimua na kuburudisha.
7. Kupitisha muda haswa watoto wanaposubiri chakula kiive

## Sifa za Mtambaji wa Hadithi

Msimulizi wa hadithi pia huitwa **mtambaji**, **fanani** au **mganaji**.

- Huwa mchangamfu na mcheshi kwa hadhira yake ili kuwafanya wapendezwe na hadithi
- Anafahamu utamaduni wa jamii yake.
- Anaifahamu hadhira yake vizuri na kusimulia kulingana na mapendeleo yao. wasichana au wavulana? vijana au wazee?
- Huwa na uwezo wa **ufaraguni** - uwezo wa kubadilisha sehemu fulani za sanaa bila kujifunga na muundo asilia.
- Mwenye kumbukumbu nzuri - uwezo wa kukumbuka
- Mwenye uwezo wa kuigiza kwa kutumia viungo vyake, uso (ishara-uso) na sauti(kiimbo)
- Mwenye uwezo wa kujenga taharuki kwa kusita kidogo ili kuvuta nadhari ya hadhira yake.
- Hushirikisha hadhira yake katika nyimbo n.k
- Mlumbi hodari na mkwasi wa lugha.
-

# Khurafa

| **KHURAFA** | |
|---|---|
| **Pia Huitwa** | • Hurafa<br>• Khurafa<br>• Hadithi za Wanyama |
| **Kiingereza** | Animal Narratives |
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera** | Hadithi (au Ngano) |
| **Prev** | Hadithi za Mtanziko |
| **Next** | Hekaya |

Hurafa au Khurafa ni hadithi ambazo wahusika wake huwa ni wanyama. Hadithi hizi hunuia kuangazia tabia za kibinadamu kupitia kwa wanyama. Hadithi nyingi huwa ni za khurafa ambapo wanyama hupewa uwezo wa kibinadamu wa kuongea, kufanya

kazi, kufikiri na nyinginezo.

Kwa kuwa wahusika wote katika hadithi za aina hii ni wanyama kutoka mwanzo hadi mwisho, hatuwezi kusema kwamba mbinu ya uhuishaji/tashihisi imetumika.

---

## Sifa za Khurafa

1. Wahusika wake ni wanyama wenye uwezo wa kuongea na kufanya kama binadamu
2. Hurejelea maswala yanayopatikana katika jamii zetu kama utendaji kazi, ukuzaji uchumi, uongozi, utangamano katika jamii, n.k
3. Funzo lake huwa wazi kv tamaa, ujinga n.k

---

## Umuhimu wa Khurafa

1. Kuburudisha hadhira
2. Kuelimisha watoto kuhusu wanyama mbalimbali na sifa zao
3. Kukuza maadili katika jamii
4. Kuelekeza na kunasihi
5. Kupitisha muda

---

## Mifano

| MNYAMA | SIFA |
|---|---|
| Sungura | tabia za ujanja - sungura huwakilisha watu wasiopenda kuchoka/kufanya kazi lakini hutumia ujanja wao kula jasho la wengine, au kuwaangamiza adui zao. |
| Simba | kwa mara nyingi simba hutumika kama kiongozi/mfalme - huwakilisha watu wenye ukali katika jamii, ambao wakiongea husikika na huogopewa sana. |
| Fisi | Ni mhusika mwenye tamaa na ulafi ambaye fikira zake zimetawaliwa na tamaa yake. Fisi hutumika kuwakilisha wanadamu wazembe na wajinga, wasiopenda kufikiria sana kwani mawazo yao yamejikita katika tamaa zao. |
| Nyani | Anapotumika katika hadithi, hudhihirisha hekima na uwezo wa kufanya uamuzi wa busara. Nyani hutumika sana kama hakimu na huwakilisha viongozi wenye hekima katika jamii. |
| Nyoka | ni mnyama mwenye hila na huwakilisha watu wenye hila katika jamii. |
| Kobe | huwakilisha watu wanyamavu, ambao japo wanajua kufanya kitu, hawapendi kuchangia, lakini mwisho huibuka washindi; watu wasiokimbilia kufanya mambo |
| Ndovu | huwakilisha watu wenye kimbelembele, ambao hujisifu na kujitafutia umaarufu. Watu wa aina hii hupenda kuwa katika msitari wa mbele japo huenda hawana ujuzi wa kutosha katika jambo lilo. |

# Hekaya

---

**HEKAYA**

| | |
|---|---|
| **Pia Huitwa** | Hadithi za Wanyama |
| **Kiingereza** | Animal Narratives |
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera** | Hadithi / Ngano |

**Next** Usuli / Visaviini

Hekaya ni hadithi ambazo huwa na mhusika mmoja mjanja au mwerefu kuliko wenzake. Mhusika huyu hutumia ujanja kujinufaisha kutoka kwa mhusika mwengine anayedanganyika kwa upesi. Kwa mfano, Hekaya za Abunuwasi, hadithi za sungura mjanja n.k

## Sifa za Hekaya

1. Huwa na mhusika mmoja mjanja anayewahadaa wenzake.
2. Mhusika mjanja hunufaika kutoka kwa wengine japo hastahili.
3. Ni hadithi fupi yenye funzo Fulani

## Umuhimu wa Hekaya

1. Kuburudisha hadhira
2. Kutoa mafunzo
3. Kutahadharisha
4. Kuelekeza na kunasihi
5. Kupitisha muda

## Mifano

1. Hadithi za Sungura na Fisi
2. Hadithi za Abunuwasi

# Ngano za Usuli (Visaviini)

**USULI**

| | |
|---|---|
| **Pia Huitwa** | Visaviini |
| **Kiingereza** | Etiological Narratives |
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera** | Hadithi / Ngano |

**Prev** Hekaya
**Next** Visasili

Ngano za usuli husimulia asili au chanzo cha dhana fulani. Visasili hukusudia kuelezea kwa nini jambo fulani hutokea au kwa nini vitu huwa kama vilivyo. Kwa mfano kwa nini fisi huchechemea, kwa nini kobe hutembea polepole n.k. Hujibu swali: *Kwa nini jambo fulani huwa jinsi lilivyo?*

---

**Tanbihi:** Tofauti kati ya visasili na usuli(visaviini) ni kwamba visasili huhusisha jamii fulani, mila, imani na matukio ya kiada kama vile kifo, tohara n.k ilhali ngano za usuli huelezea kwa nini mambo fulani hufanyika bila kuhusisha jamii au imani.

---

## Sifa za Usuli

1. Hueleza aili ya dhana/hali fulani ulimwenguni.
2. Huwa na mwanzo maalum - kuonyesha kwamba katika zama za kale dhana inayorejelewa, haikuwa vile ilivyo sasa.
   Mfano:
    1. Hapo zamani za kale, kobe alikuwa na ngozi laini kama wanyama wengine...
3. Huwa na mwisho maalum - kuthibitisha kwamba yaliyosimuliwa katika hadithi hiyo ndiyo yaliyopelekea kuwepo kwa hali hiyo.
   k.m:
    1. *...Hii ndiyo sababu ngozi ya kobe ina magamba.*
    2. *... Tangu siku hiyo fisi huchechemea.*
    3. *... na hadi wa leo kuku hutazama juu anapokunywa maji.*
4. Hurejelea dhana zinazopatikana katika ulimwengu wa sasa.

## Umuhimu wa Usuli

1. Kuelimisha watoto kuhusu mazingira na dhana mbalimbali
2. Kutafuta maelezo ya mambo yanayochukuliwa kuwa ya kawaida.
3. Kuelekeza na kunasihi
4. Kuburudisha hadhira
5. Kukuza uwezo wa kufikiri
6. Kupitisha muda

---

## Mifano

1. Kwa nini fisi huchechemea
2. Kwa nini ngozi ya Kobe ina magamba
3. Kwa nini chura ana mabaka katika ngozi yake
4. Kwa nini kanga hana manyoya
5. Kwa nini Paka na panya ni maadui

# Visasili (Visa-asili)

---

| **VISASILI** | |
|---|---|
| **Pia Huitwa** | • Visaasili |

- Visa-asili

| | |
|---|---|
| **Kiingereza** | Myths |
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera** | Hadithi / Ngano |

Visasili ni ngano za kihistoria zinazoeleza chimbuko /**asili** ya jamii/kabila fulani; tamaduni mbali mbali katika jamii ile na namna jamii hiyo ilivyofika katika eneo lake la sasa. Visasili husaidia kuelezea asili ya mambo yasiyoelezekakama vile mauti, jando, tohara, ndoa na tamaduni/imani nyinginezo.
**Tanbihi:** Tofauti kati ya visasili na usuli(visaviini) ni kwamba visasili huhusisha jamii fulani, mila, imani na matukio ya kiada kama vile kifo, tohara n.k ilhali ngano za usuli huelezea kwa nini mambo fulani hufanyika bila kuhusisha jamii au imani.

## Sifa za Visasili

1. Huelezea chimbuko la jamii fulani
2. Matokeo yake hufanyika mwanzoni (k.v mwanzo wa dunia)
3. Aghalabu huhusisha miungu, malaika n.k
4. Kuburudisha

## Umuhimu wa Visasili

1. Kutafuta jibu kwa maswali yanayotatiza
2. Kuhifadhi historia na imani ya jamii
3. Kuunganisha jamii
4. Kuwasilisha mila na desturi za jamii

## Mifano

1. Asili ya jamii ya Wamaasai
2. Asili ya Wagikuyu

# Mighani au Visakale

**MIGHANI**

| | |
|---|---|
| **Pia Huitwa** | • Visakale<br>• Hadithi za Mashujaa |
| **Kiingereza** | Legend Narratives |
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera** | Hadithi / Ngano |
| **Prev** | Visasili |
| **Next** | Hadithi za Mazimwi |

Visakale ni hadithi za mashujaa wanaosifiwa katika jamii. Aghalabu mashujaa hawa walipigania jamii zao katika vita dhidi ya jamii nyingine au vita vya ukombozi. Shujaa katika visakale huitwa **jagina**. Maadui wa mashujaa huitwa **Majahili**

## Sifa za Mighani

1. Hutumia chuku kusifia matendo na uwezo wa shujaa.
2. Majagina huwa na uwezo wa **ukiamaumbile** (uwezo unaozidi wa binadamu)
3. Huwa ni vigumu sana kwa shujaa kuuawa minghairi ya idadi ya maadui wake
4. Shujaa huwa na siri kuu ya nguvu zake (kama nguvu kuwa kwenye kivuli, nywele, n.k)
5. Jagina hupigania haki za jamii yake
6. Jamii ya jagina huwakilisha wema ilhali maadui wao huwakilisha ubaya.
7. Jagina hufa mwishoni, haswa baada ya kusalitiwa na mtu wake.
8. Hadithi hizi huaminika kuwa za kweli ama zenye kiwango fulani cha ukweli; kwamba mashujaa hao walikuwa.

## Sifa za Jagina (Shujaa)

1. Huwa na nguvu zinazotokana na siri fulani
2. Wana uwezo wa ukiamaumbile
3. Hupigania haki za jamii yao
4. Huwa na kimo kisichokuwa cha kawaida k.v mfupi sana, mrefu sana n.k
5. Aghalabu huwa watu wema kulingana na maadili ya jamii zao.

## Umuhimu wa Visakale

1. Kuunganisha jamii
2. Kuhifadhi historia ya jamii
3. Kuelimisha, kunasihi na kuelekeza
4. Kuburudisha
5. Kupitisha muda

---

## Mifano ya Majagina

| JAGINA | KABILA | |
|---|---|---|
| Mekatilili wa Menza | Giriama | Mwanamke aliyeongoza wanandi dhidi ya wakoloni |
| Fumo wa Linyongo | Wapate | Vita dhidi ya Sultani wa Pate |
| Kinjeketile Ngwale | Wamatumbi | Majimaji Rebellion |
| Luanda Magere | Luo | Vita dhidi ya Wanandi |
| Koitalel arap Samoei | Nandi | Nandi Rebellion |
| Shaka | Zulu | Aliongezea ufalme wa Kizulu |

# Ngano za Mazimwi

| NGANO ZA MAZIMWI | |
|---|---|
| **Kiingereza** | Orge Narratives |
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera** | Hadithi / Ngano |

Hizi ni ngano ambazo baadhi ya wahusika wake ni majitu makubwa yenye uwezo **ukiamaumbile** (uliozidi wa kawaida).

Mazimwi ni viumbe waliobuniwa na binadamu ambao wanaweza changanya sifa zi binadamu, za mnyama na za shetani. Aghalabu mazimwi hufanya maovu kama vile kula watu.

## Sifa za Mazimwi

1. Mazimwi yanaweza kuwa na mchanganyo wa sifa za kibinadamu, za wanyama na za kishetani.
2. Mazimwi huwa na maumbile yasiyokuwa ya kawaida kama vile pembe, mikono mitatu, jicho la nyuma n.k
3. Mazimwi yana uwezo wa kujibadilisha kutoka umbo moja hadi jingine. k.v mti, msichana, kisima, nyoka n.k
4. Mazimwi huwa adui kwa wanadamu na huwaangaisha sana kwa kuwala, kuwatisha, kuwaibia, kuwaharibia mali na kuvuruga amani katika jamii.
5. Wanaohangaishwa sana na mazimwi ni wanawake, watoto na watu wanaotembea usiku au kwenda katika maeneo fulani.
6. Aghalabu zimwi hushindwa nguvu na kufa. Kwa mara nyingi, watu walioliwa/kumezwa na jitu hutokeza kabla ya kifo chake.
7. Aghalabu, hadithi za mazimwi huwa na mwisho maalum, k.v tangu siku hiyo waliishi raha mustarehe.

## Umuhimu wa Ngano za Mazimwi

1. Kutahadharisha watu wawe makini.
2. Kutuonya dhidi ya maovu kama vile ulafi, tamaa n.k
3. Kuhimiza utiifu
4. Kuburudisha
5. Kupitisha muda

# Ngano za Mtanziko

---

**NGANO ZA MTANZIKO**

| | |
|---|---|
| **Kiingereza** | Dilemma Narratives |
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera** | Hadithi / Ngano |

Hadithi za mtanziko ni ngano ambazo mhusika hulazimika kuchagua mojawapo ya hali mbili ambazo ni ngumu kuamua ili kupata suluhisho la jambo fulani. Uamuzi wowote anaoufanya huwa na mabaya yake. Ni jukumu la mhusika kufikiri sana kabla ya kufanya uamuzi

---

## Sifa za hadithi za Mtanziko

1. Kuna mambo mawili ambayo mhusika analazimika kuchagua moja.
2. Uamuzi huwa mgumu kwa vile kila chaguo huwa na matokeo yake mabaya
3. Mhusika huwa na tatizo moja kuu ambalo linaweza tu kutatuliwa na uamuzi atakaofanya.
4. Aghalabu hutumia mbinu ya taharuki
5. Aghalabu huishia kwa swali k.v, *Ingekuwa wewe, ungefanyaje?*

## Umuhimu wa Hadithi za Mtanziko

1. Kukuza uwezo wa kufikiri wa hadhira
2. Kunasihi hadhira wafanye uamuzi wa busara.
3. Kuzua mjadala nyeti katika jamii
4. Kuburudisha hadhira

5. Kupitisha muda

## Mifano

1. Zimwi linakuamuru ulipatie mama yako aliyekuzaa na kukulea au mke wako unayempenda sana

# Nyimbo Katika Fasihi Simulizi

**NYIMBO**

**Utanzu wa** Fasihi Simulizi

**Kiingereza** Songs

**TANZU ZA FASIHI**

**MBINU ZA SANAA**

Nyimbo ni aina ya sanaa katika fasihi ambayo hutumia lugha teule, sauti na kiimbo maalum.

Aghalabu nyimbo hutumia ala za mziki kama vile ngoma. Nyimbo zinaweza kuimbwa na mtu mmoja au zaidi.

Wimbo hugawanywa katika beti na mishororo. Nyimbo nyingi huwa na **kiitikio** au mstari ambao hurudiwa rudiwa.

## Sifa za Nyimbo

1. Hutumia kiimbo au sauti maalum
2. Huweza kuendamana na ala za muziki
3. Huimbwa na mtu mmoja au watu wengi; wakati mwingine nyimbo huimbwa kwa kupokezanwa.
4. Hutumia lugha ya mkato
5. Hurudiarudia (kukariri) maneno ili kusisitiza ujumbe katika wimbo

## Umuhimu wa Nyimbo katika Fasihi Simulizi

1. Kuburudisha
2. Kuelimisha, kufunza, kuonya, kuelekeza
3. Kuliwaza
4. Kusifia kitu au mtu katika jamii
5. Kuunganisha jamii
6. Kudumisha/kuhifadhi tamaduni za jamii
7. Kukuza talanta na sanaa katika jamii
8. Hutumika katika mbinu nyingine za fasihi kama vile hadithi

## Vipera/Aina za Nyimbo

### Kulingana na Muundo:

- Mashairi
- Maghani

### Kulingana na Ujumbe/Maudhui:

#### Nyimbo za Ndoa

Nyimbo za harusi huimbiwa bwana na bibi harusi kuwapongeza na kuwapa heko kwa kufunga ndoa yao. Aidha nyimbo hizi huwapa wawili hao mawaidha ya kutunza familia na watoto wao ili waishi pamoja.

**Nyimbo za Jandoni/Tohara**

huimbwa na vijana wanapopashwa tohara. Nyimbo hizi huonyesha ushujaa, na kuashiria kutoka kwamba anayetahiriwa amekuwa mtu mzima sasa.

**Hodiya/Wawe**

Hizi ni nyimbo ambazo huimbwa na watu wanapofanya kazi ili kuwatia bidii wafanye kazi bila kuhisi machofu.

**Kimai**

Nyimbo za Mabaharia - Hizi ni nyimbo za wanabahari wanaposafiri baharini.

**Nyimbo za Mazishi/Huzuni/Simanzi**

Hizi ni nyimbo za kuliwaza na kuwapa pole walioachwa na marehemu. Nyimbo hizi huwapa matumaini waombolezaji.

**Nyimbo za Kidini**

Hizi ni nyimbo ambazo huimbwa kumsifia Mungu, kuomba au kutoa mafunzo ya kidini.

**Nyimbo za Kisiasa**

Hizi ni nyimbo za kuwasifia viongozi wa kisiasa

**Nyimbo za Kizalendo**

Nyimbo za huonyesha uzalendo kwa kusifia taifa/nchi

**Nyimbo za Mapenzi**

Katika nyimbo za mapenzi, mwimbaji huimba kwa kumsifia mpenzi wake hasa kwa urembo na tabia zake.

# Maigizo

---

| **MAIGIZO** | |
|---|---|
| **Utanzu wa** | Fasihi Simulizi |
| **Vipera vya Maigizo** | • Michezo ya Kuigiza<br>• Miviga<br>• Ngomezi<br>• Malumbano ya Utani<br>• Ulumbi<br>• Soga<br>• Vichekesho<br>• Maonyesho ya Sanaa |

---

Maigizo ni sanaa katika fasihi simulizi ambayo watendaji huwa ndio wahusika. Maigizo hayasimuliwi kama mbinu nyingine za fasihi. Wahusika ndio huzungumza katika sehemu zao mbalimbali.

---

Mifano:

1. Michezo ya Kuigiza (Jukwaani) - Haya ni maigizo ya jukwaani ambapo watendaji huiga maneno na matendo ya wahusika mbele ya hadhira.
2. Miviga - Miviga ni sherehe mbalimbali katika jamii fulani. Watu hujumukika na sherehe hizi kulingana na tamaduni zao

3. Ngomezi - ni sanaa ya ngoma. Midundo mbalimbali ya ngoma hutumika kuwasilisha ujumbe mbalimbali.
4. Malumbano ya Utani - Malumbano ya utani ni mashindano ya kuongea jukwaani baina ya watu wa makundi au jamii mbili ambayo hutumia kejeli na chuku kukejeli tabia mbaya katika jamii au kundi fulani
5. Ulumbi - Ulumbi ni uwezo wa kipekee wa kuzungumza mbele ya hadhira. Mtu mwenye uwezo huo wa kipekee wa kuzungumza jukwaani huitwa mlumbi.
6. Soga - Soga ni mazungumzo baina ya watu wawili au zaidi ambayo aghalabu huwa hayana mada maalum.
7. Vichekesho - Vichekesho ni aina ya sanaa ya fasihi simulizi ambayo watu hutoa vihadithi vifupi au sentensi zenye uwezo wa kuwafanya wasikilizaji wacheke.
8. Maonyesho ya Sanaa - Maonyesho huhusisha watu wa jamii au kundi fulani wanaoonyesha taaluma, ujuzi au sanaa yao kwa watazamaji.

# Michezo ya Kuigiza

| MICHEZO YA KUIGIZA | |
|---|---|
| **Pia Huitwa** | Michezo ya Jukwaani |
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera cha** | Maigizo |

Haya ni maigizo ya jukwaani ambapo watendaji huiga maneno na matendo ya wahusika na kuyasema wakiwa kwenye jukwaani. Jukwaa hutayarishwa ili kuiga mazingira ya tamthilia au tukio wanaloliigiza.

**Content**


- Sifa za Michezo ya Kuigiza
- Umuhimu wa Michezo ya Kuigiza


## Sifa za Michezo ya Kuigiza

1. Huwa na wahusika ambao huwakilishwa na watendaji.
2. Hufanyika kwenye jukwaa mbele ya hadhira
3. Huhitaji kumbukumbu ili kukumbuka maneno ambayo mhusika anapaswa kusema katika jukwaa
4. Vitambaa au mwangaza hutumiwa ili kuashiria kubadilika kwa mazingira au wakati
5. Hutumia mbinu za lugha kama vile chuku, tanakali za sauti, tamathali na nyinginezo
6. Hujumulisha aina nyingine za sanaa kama vile ushairi na nyimbo.

## Umuhimu wa Michezo ya Kuigiza

1. Huburudisha
2. Huelimisha
3. Hukuza uwezo wa kukumbuka kwa watendaji

# Miviga

| MIVIGA | |
|---|---|
| **Pia Huitwa** | Sherehe |
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera cha** | Maigizo |

Miviga ni sherehe mbalimbali katika jamii fulani. Watu hujumukika na sherehe hizi kulingana na tamaduni zao. Watu mbalimbali katika jamii huwa na majukumu tofauti tofauti. Miviga huandamana na nyimbo, vyakula na mawaidha kutoka

kwa wazee. Mifano ya miviga ni kama vile Sherehe za ndoa, mazishi, tohara n.k

### Sifa za Miviga

1. Huandamana na nyimbo zinazohusiana na sherehe hiyo kwa mfano nyimbo za mazishi, ndoa n.k
2. Ngoma mbalimbali huchezwa
3. Huwa na vyakula vya kienyeji
4. Aghalabu kina mama hupewa kazi za upishi na burudani
5. Wazee hutoa mafunzo, mawaidha kwa vijana

### Umuhimu wa Miviga

1. Huleta jamii pamoja na kuunganisha watu katika jamii
2. Watu hupata mafunzo kutoka kwa wazee katika jamii
3. Hudumisha tamaduni katika jamii
4. Huburudisha - kwa mfano sherehe zinapohusisha nyimbo na michezo ya kuigiza
5. Huliwaza - kwa mfano wakati wakati wa huzuni kama vile mazishi

# Ngomezi

**NGOMEZI**

| | |
|---|---|
| **Pia Huitwa** | Sanaa ya Ngoma |
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera cha** | Maigizo |

Ngomezi ni sanaa ya ngoma. Midundo tofauti tofauti ya ngoma hutumika kuwakilisha ujumbe au maana fulani. Ngoma zilitumika sana kabla ya teknolojia ya barua na simu. Wataalam wa ngoma walipiga ngoma kwa milio mbalimbali kufahamisha jamii kwa jambo fulani limefanyika kwa mfano kuingia kwa adui, moto, mtoto anapozaliwa n.k

### Sifa za Ngomezi

1. Hutumia midundo mbalimbali ya ngoma kupitisha ujumbe fulani
2. Huhitaji mtaalam wa ngoma
3. Maana ya midundo mbalimbali hubadilika kutoka kwa jamii moja hadi nyingine, hivyo basi ni vigumu kwa jamii-adui kutambua ujumbe wake

### Umuhimu wa Ngomezi

1. Kupitisha ujumbe
2. Kutahadharisha jamii dhidi ya adui
3. Kuburudisha
4. Kuhifadhi tamaduni za jamii

# Malumbano ya Utani

**MALUMBANO YA UTANI**

| | |
|---|---|
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera cha** | Maigizo |

Malumbano ya utani ni mashindano ya kuongea jukwaani baina ya watu wa makundi au jamii mbili ambayo hutumia kejeli na chuku kukejeli tabia mbaya katika jamii au kundi fulani. Watu husimama jukwaani na kushindana kwa maneno.

### Sifa za Malumbano ya Utani

1. Hutumia mzaha na vichekesho
2. Hutumia kinaya na kejeli ili kuangazia ukweli fulani katika jamii

### Umuhimu wa Malumbano ya Utani

1. Kurekebisha mambo mabaya katika jamii
2. Kuburudisha
3. Kupitisha muda

# Ulumbi

---

**ULUMBI**

**Utanzu wa Fasihi** Fasihi Simulizi

**Kipera cha** Maigizo

Ulumbi ni uwezo wa kipekee wa kuzungumza mbele ya hadhira. Mtu mwenye uwezo huo wa kipekee wa kuzungumza jukwaani huitwa mlumbi. Walumbi husifika sana kwa kuzungumzia mambo yanayoathiri jamii.

### Sifa za Mlumbi

1. Ana uwezo wa kushawishi watu kuhusu ujumbe anaopitisha.
2. Huwa mkwasi wa lugha anayeifahamu vizuri lugha yake.
3. Hutumia lugha ya kuvutia na kumakinisha hadhira
4. Anaifahamu sana hadhira yake na maswala yanayoiathiri.
5. Ni kiongozi.

### Umuhimu wa Ulumbi katika jamii

1. Kuhamasisha jamii kuhusu mambo yanayowakabili.
2. Kuunganisha watu watekeleze jambo fulani kwa pamoja
3. Kuburudisha

# Soga (Mazungumzo)

---

**SOGA / MAZUNGUMZO**

**Pia Huitwa**
- Mazungumzo
- Gumzo

**Utanzu wa Fasihi** Fasihi Simulizi

**Kipera cha** Maigizo

Soga ni mazungumzo baina ya watu wawili au zaidi ambayo aghalabu huwa hayana mada maalum. Aghalabu soga huwa na vichekesho vingi, mzaha na kejeli. Nia yake huwa kuburudisha na kupitisha wakati.

### Sifa za Soga

1. Soga huwa na vichekesho na mzaha mwingi
2. Mada hubadilikabadilika kutoka wakati mmoja hadi mwingine
3. Haihitaji taaluma yoyote ya kisanaa
4. Inaweza kufanyika mahali popote - njiani, sebuleni, katika vyumba vya burudani n.k

### Umuhimu wa Soga

1. Kupitisha wakati hasa watu wanaposubiri jambo fulani lifanyike kama vile chakula kiive
2. Kuburudisha
3. Kuunganisha jamii

# Vichekesho

| VICHEKESHO | |
|---|---|
| **Pia Huitwa** | Vivunja Mbavu |
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera cha** | Maigizo |

Vichekesho ni aina ya sanaa ya fasihi simulizi ambayo watu hutoa vihadithi vifupi au sentensi zenye uwezo wa kuwafanya wasikilizaji wacheke. Vichekesho huhitaji ubunifu mwingi ili kutaja jambo litakalowavunja bavu hadhira.

### Sifa za Vichekesho

1. Huwa na uwezo wa kutekenya hisia hadi mtu acheke.
2. Aghalabu vichekesho huwa vifupi
3. Hutumia mifano ya vitu vinavyojulikana wazi na hadhira katika mazingira/mandhari yao.
4. Hutumia mbinu ya kejeli na chuku sana.

### Umuhimu wa Vichekesho

1. Kuburudisha
2. Kupitisha wakati

# Tungo Fupi

| TUNGO FUPI | |
|---|---|
| **Utanzu wa** | Fasihi Simulizi |
| **Vipera vya Tungo Fupi** | • Methali<br>• Vitendawili<br>• Mafumbo<br>• Semi (Nahau na Misemo)<br>• Vitanza Ndimi na Vichezea Maneno<br>• Lakabu<br>• Misimu |
| **Maigizo** | Hadithi / Ngano |

Tungo Fupi ni kipera cha Fasihi Simulizi kinachojumulisha sanaa simulizi zinazoundwa kwa maneno machache; sentensi moja au mbili hivi. Tungo Fupi nyingi huwa na sehemu mbili na aghalabu huhitaji kujibizana ambapo mtu mmoja hutoa pendekezo au swali; halafu mtu mwengine hutoa jawabu - k.m vitendawili na mafumbo. Baadhi ya tungo fupi husemwa na mtu mmoja tu kama vile methali.

Aghalabu vipera vyote vya tungo fupi hutumiwa katika kazi nyingine za fasihi ( na lugha kwa ujumla ) kama mapambo ya lugha.

### Vipera vya Tungo Fupi

1. Methali
   Methali ni tungo fupi za sentensi moja ambazo hutoa

funzo fulani kwa njia ya mafumbo. Methali huwa na sehemu mbili. Sehemu ya kwanza hutoa hoja nayo sehemu ya pili hutoa suluhisho. Methali hutumika kwa minajili ya kutoa funzo kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Methali nyingine huhitaji hekima ili kujua maana yake.

2. Vitendawili
   Vitendawili ni tungo fupi ambazo huwa na swali fupi na jibu kwa makusudi ya kupima ufahamu wa hadhira kuhusu mazingira yake. Anayetoa kitendawili huulizia swali lake kwa kutoa maelezo mafupi yanayorejelea umbo la kitu hicho, sauti, harufu au kukifananisha na kitu kingine. Anayejibu huhitajika kufikiria haraka na kutoa jawabu ambalo huwa la neno moja au maneno mawili hivi. Vitendawili huwa na mianzo maalum kulingana na jamii yake.
3. Mafumbo
   Mafumbo hutumika kuupima uwezo wa mtu kufikira na kufumbua swali ambalo huwa na maelezo marefu. Majibu ya mafumbo huhitaji maelezo na aghalabu hukusudia kujua jinsi mtu anavyoweza kutatua tatizo fulani ambalo linahitaji kufikiria sana.
4. Vitanza Ndimi
   Vitanza ndimi huwa ni sentensi zinazotumia maneno yanayomkanganya msomaji katika matamshi. Vitanza ndimi huhitaji kutamkwa haraka haraka na kurudiwa rudiwa mara kadhaa kwa kusudi la kukuza uwezo wa kutamka.
5. Vichezea Maneno
   Ni maneno yanayokaribiana kimatamshi au kimaana hutumika katika sentensi moja kama njia ya kuonyesha ukwasi wa lugha au kuburudisha. Pia hutumika kama vitanza ndimi.
6. Misimu
   Misimu ni maneno ambayo huzuka miongoni mwa kundi fulani katika jamii na hueleweka tu miongoni mwa watu katika kundi hilo. Misimu hukua na kutoweka baada ya muda.
7. Lakabu
   Lakabu ni majina yanayobandikwa watu kutokana na sifa zao, maumbile, hulka au mambo yanayowahusu. Lakabu pia ni mbinu ya sanaa.
8. Semi (Nahau na Misemo)
   Semi ni mafungu ya maneno ambayo hutumika kuleta maana tofauti na maana halisi ya maneno yaliyotumika. Semi hutumika kuficha maneno makali kwa kutumia maneno mengine. Aidha semi zinaweza kutumika tu kwa minajili ya kupamba lugha. Kuna aina mbili za semi: **Nahau** na **misemo**

# Methali Katika Fasihi

---

| **METHALI** | |
|---|---|
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera cha** | Tungo Fupi |
| **Kiingereza** | • Proverbs<br>• Wise-Sayings |

---

| | |
|---|---|
| **Tungo Fupi** | Vitendawili |
| **Mbinu za Lugha** | Maswali ya Balagha |

Methali ni tungo fupi za kisanaa ambazo hutoa wosia/nasaha kwa lugha ya mafumbo.

## Sifa za Methali

1. **Huwa na maana ya ndani na ya nje.**

   Maana ya ndani huwa fiche na huhitaji hekima kuitambua. Maana ya juu huwa wazi kwani hurejelea vitu vinavyojulikana vizuri.

1. Dua la kuku halimpati mwewe =>
    - maana ya juu i wazi kwamba kilio na laana za kuku haziwezi kumwathiri mwewe alimnyang'anya kifaranga.
    - Maana ya ndani ni kwamba kilio cha mnyonge asiye na uwezo hakiwezi kumhangaisha mwenye nguvu/ mtesi wake.

**2. Methali huwa na vipande viwili**

1. Mtaka cha mvunguni, sharti ainame
2. Mpanda ngazi, hushuka
3. Hasira, hasaraMifano ya Methali

**3. Baadhi ya methali hutumia mbinu za lugha**

1. **Takriri** => kinga na kinga ndipo moto huwakapo
2. **Istiara** => mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi
3. **Tashbihi** => mapenzi ni kama kikohozi, hayafichiki
4. **Kejeli** => Ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno
5. **Chuku** => maji ya kifuu bahari ya chungu
6. **Tashihisi** => sikio la kufa halisikii dawa

**4. Methali huwa na mazingira**

1. **Ukulima** => mchagua jembe si mkulima
2. **Uvuvi** => hasira za mkizi, furaha ya mvuvi
3. **Elimu** => elimu ni mwangaza gizani hung'aa
4. **Familia** => Uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi

**5. Baadhi ya methali ni refu, nyingine ni fupi**

1. Cha mkufuu mwanafuu ha na akila hu, cha mwanafuu mkufuu hu na akila ha. (refu)
2. Akiba haiozi (fupi)

**6. Methali huwa na wakati - kuna methali za kale na za kisasa**

1. Mti mkuu ukigwa wana wa nyuni huyumba (kale)
2. Mti mkuu ukianguka ndege huwa mashakani (kisasa)

**7. Methali huwa na funzo**

Hakuna methali isiyokuwa na funzo lake.

**8. Baadhi ya Methali huwa na Ukinzani - kuwepo kwa methali nyingine inayopinga maana ya hiyo**

1. Ngoja ngoja huumiza matumbo; mstahimilifu hula mbivu
2. fuata nyuki ufe mzingani; fuata nyuki ule asali
3. mavi ya kale hayanuki; mavi ya kale hayaachi kunuka

**9. Baadhi ya Methali huwa na maana sawa**

1. Haraka haraka haina baraka;
   Polepole ndio mwendo;
   Simba mwenda pole ndiye mla nyama
2. Mchagua jembe si mkulima;
   Mshoni hachagui nguo

## Umuhimu wa Methali

1. Methali huonya/hutahadharisha watu katika jamii dhidi ya maovu. k.v. *Usipoziba ufa utajenga ukuta*
2. Methali hutoa mafunzo k.v bahari haivukwi kwa kuogelea
3. Methali hutumiwa na waandishi, wazungumzaji na katika kazi mbali mbali za sanaa kama mapambo ya lugha
4. Hutumika kutoa mawaidha katika jamii - mfano: *asiyefunzwa na mama hufunzwa na ulimwengu*
5. Hutumika kuunganisha jamii pamoja. Kuna methali nyingi zinazosisitiza umoja k.m *Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu; kidole kimoja hakivunji chawa.*

# Vitendawili

---

**VITENDAWILI**

**Utanzu wa Fasihi** Fasihi Simulizi

**Kipera cha** Tungo Fupi

| | |
|---|---|
| **Kiingereza** | Riddles |
| **Prev** | Methali |
| **Next** | Mafumbo |

Vitendawili ni tungo fupi ambazo huwa na swali fupi lisilo wazi na jibu kwa makusudi ya kupima ufahamu wa hadhira kuhusu mazingira yake. Anayetoa kitendawili huulizia swali lake kwa kutoa maelezo mafupi yanayorejelea umbo la kitu hicho, sauti, harufu au kukifananisha na kitu kingine. Anayejibu huhitajika kufikiria haraka na kutoa jawabu ambalo huwa la neno moja au maneno mawili hivi. Vitendawili huwa na mianzo maalum kulingana na jamii yake.

## Sifa za Vitendawili

1. Vitendawili huwa na mwanzo maalum : Kitendawili – tega
2. Hupitishwa baina ya watu wawili – anayetega na anayetegua
3. Vitendawili huwa na muundo maalum wa kuendelezwa (utangulizi, swali, (majaribio ya) jibu; wanaotegua wakishindwa anayetega huwa ameshinda, huitisha apewe mji/zawadi na kisha kutoa jibu)
4. Huwa na vipande viwili – swali na jibu. Mfano: Kila niendapo ananifuata – kivuli.
5. Hutumia mbinu ya jazanda, kufananisha vitu viwili moja kwa moja. K.v. Nyumba yangu haina mlango – yai (yai limelinganishwa moja kwa moja na nyumba isiyo mlango)
6. Hurejelea vitu vinavyopatikana katika mazingira na vinavyojulikana sana
7. Vitendawili vilitegwa wakati maalum, hasa wa jioni
8. Vitendawili hutumia tamathali za usemi (mbinu za lugha) kama istiara, tashihisi, tashbihi, jazanda, chuku, tanakali za sauti, n.k
9. Vitendawili huwa na jibu maalum.

## Aina za Vitendawili

**a) Vitendawili sahili**

ni vifupi na huwa na na muundo mwepesi kueleweka. K.v.

**b) Vitendawili mkufu**

huwa na vipande vinavyofuatana na kila kipande huwa na uhusiano na kipande kilichotangulia. Mfano – nikisimama anasimama, nikiketi anaketi, nikiondoka huondoka pia

**c) Vitendawili vya tanakali**

hutumia tanakali za sauti Mfano: Drrrrrrh mpaka ng'ambo – buibui; huku ng'o na kule ng'o.

**d) Vitendawili sambamba**

huwa na maelezo marefu (kama hadithi fupi) halafu jibu lake huwa ni refu pia (kama mafumbo)

## Umuhimu wa vitendawili

1. Vitendawili huburudisha kwani hutegwa kwa njia ya uchangamfu na ushindani.

2. Huwaleta watu pamoja (huunganisha jamii) kwani vinapotegwa watu hukusanyika pamoja.
3. Vitendawili huhamasisha watu kuhusu mazingira yao kwani hulenga vitu vinavyopatikana katika jamii hiyo.
4. Vitendawili hukuza uwezo wa kufikiria/kukumbuka kwani anayetoa jibu huhitajika kukumbuka jibu la kitendawili.
5. Vitendawili hukuza na kuhifadhi tamaduni kwa maana hupokezanwa kutoka kizazi hadi kizazi.
6. Vilitumika kupitisha wakati na kuwafanya watoto wasilale mapema kabla ya chakula kuwa tayari.

# Mafumbo

---

| **MAFUMBO** | |
|---|---|
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera cha** | Tungo Fupi |
| **Kiingereza** | Riddles |

Mafumbo ni aina ya tungo fupi ambazo huwa na maelezo yanayoishia kwa swali; kisha anayejibu huhitajika kufikiria ili kutambua jibu. Kinyume na vitendawili, majibu ya mafumbo huwa na maelezo marefu.

## Sifa za Mafumbo

1. Mafumbo huwa na sehemu mbili – sehemu ya swali na sehemu ya jibu.
2. Huwa baina ya watu wawili – anayefumba na anayefumbua (wanaofumbua)
3. Mafumbo yaliendelezwa wakati maalum.
4. Jibu la fumbo si maalum kwani kinachohitajika ni mantiki katika jibu.

---

## Umuhimu wa methali

1. Hukuza uwezo wa kufikiri ili kupata jibu.
2. Huimarisha umoja katika jamii kwani watu huja pamoja wanapofumbiana mafumbo.
3. Mafumbo huhifadhi utamaduni – hupokezanwa kutoka kizazi hadi kizazi
4. Mafumbo hutumika kama burudani
5. Hutumika kupitisha muda.

---

## Mifano ya mafumbo

1. **Fumbo:** Ajali mbaya ilitokea kati ya mpaka wa Kenya na Tanzania. Je, majeruhi walizikwa wapi?
   **Jibu:** *majeruhi hawakuzikwa, walikimbizwa hospitalini*
2. **Fumbo:** Upepo ulikuwa unavuma sana kutoka mashariki hadi magharibi. Nilikuwa nikiliendesha gari la moshi linalotumia umeme kutoka Burundi hadi Malawi. Je, moshi ulielekea upande gani?
   **Jibu:***Gari la moshi linalotumia umeme halitoi moshi*
3. **Fumbo:** Mimi na ndugu yangu tulinunua fahali mmoja kutoka sokoni. Baada ya mwaka mmoja alijifungua ndama wawili. Je kila mtu alipata wangapi?
   **Jibu:** *ndama hajifungui*
4. **Fumbo:** Juma ana vitu vitatu; mbwa, kuku na mchele anaotaka kuvusha mto. Mbwa hula kuku na kuku hula mchele. Kulingana na sheria za kuvuka daraja lile, hauwezi kuvuka ukiwa na zaidi ya vitu viwili. Je juma atatumia njia gani kuvuka?

**Jibu:** *kwanza atavusha mbwa na mchele kisha atarudi na kumchukua kuku.*

# Semi - Misemo na Nahau

| | |
|---|---|
| **SEMI - MISEMO NA NAHAU** | |
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera cha** | Tungo Fupi |
| **Kiingereza** | Colloquial Expressions |
| **VIPERA VYA SEMI** | |
| **Nahau** | Huwa na Vitenzi |
| **Misemo** | Haina Vitenzi |

Semi ni mafungu ya maneno yanayotumiwa kuleta maana nyingine badala ya maana halisi ya maneno yaliyotumika.

Kwa mfano tukisema mtu *amegonga mwamba* hatumaanishi kwamba amepiga jiwe kubwa kwa mkono au kwa kifaa chochote, bali tunamaanisha kwamba ameshindwa kuendelea katika jambo fulani.

Semi ni kipera cha tungo fupi katika fasihi simulizi; na hutumiwa katika aina nyingine za sanaa kama tamathali za lugha. Kuna fani mbili za Semi:

1. Nahau - ni semi zenye kitenzi (virai vitenzi)
2. Misemo - ni semi zisizokuwa na vitenzi

## Umuhimu wa Semi

1. Kupunguza ukali wa maneno k.m: *amega dunia* badala ya *amekufa*
2. Kupamba lugha
3. Kuhifadhi mali amali ya lugha/jamii

## Mifano ya Nahau

| NAHAU | MAANA |
|---|---|
| Kupiga moyo konde | kujituliza/kujiliwaza |
| Kujipa moyo | kujiliwaza |
| Kupiga hatua | kuendelea mbele |
| Kukata kamba | kuaga dunia |
| Kupiga darubini | kufanya uchunguzi |
| Kutupa macho | kuangalia mbali |
| Kupigwa kalamu | kufutwa kazi |
| Kuandaa meza | kutayarisha chakula |
| Kugonga mwamba | kutofanikiwa |
| Kwenda msalani | kwenda chooni |

## Mifano ya Misemo

| MSEMO | MAANA |
|---|---|
| Mkono wa birika | uchoyo |
| uzi na shindano | ushirikiano |
| Shingo upande | bila kupenda |
| kiguu na njia | mtu asiyetulia mahali pamoja |
| Mdomo na pua | karibu sana |

Lila na fila mema na mabaya

# Vitanza Ndimi na Vichezea Maneno

| **VITANZA NDIMI NA VICHEZEA MANENO** | |
|---|---|
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera cha** | Tungo Fupi |
| **Kiingereza** | • Tongue Twisters<br>• Word Play<br>• Pun |

## Vitanza ndimi

Vitanza ndimi huwa ni sentensi zinazotumia maneno yanayomkanganya msomaji katika matamshi. Vitanza ndimi huhitaji kutamkwa haraka haraka na kurudiwa rudiwa mara kadhaa kwa kusudi la kukuza uwezo wa kutamka.
k.m:

1. Shirika la reli la Rwanda lilishirikiana na shirika la reli la Libya.
2. Ni zipi zikusikitishazo?

## Vichezea Maneno

1. Ni maneno yanayokaribiana kimatamshi au kimaana hutumika katika sentensi moja kama njia ya kuonyesha ukwasi wa lugha au kuburudisha. Pia hutumika kama vitanza ndimi.
2. Nitasisitiza na nitasita kusitasita.
3. Kanga wa Mahanga mwenya matanga anatangatanga Tanga

# Lakabu

| **LAKABU** | |
|---|---|
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera cha** | Tungo Fupi |
| **Kiingereza** | Nicknames |
| **Angalia** | Majazi |

Lakabu ni majina yanayobandikwa watu kutokana na sifa zao, maumbile, hulka au mambo yanayowahusu.

Kama vile semi, lakabu ni tungo fupi ambazo zinaweza kutumika kama Mbinu za Lugha na Sanaa

Tofauti kuu kati ya lakabu na majazi ni kwamba majazi ni jina halisi la mtu ilhali lakabu ni jina la kupachikwa.

## Mifano ya Lakabu

- Katika riwaya ya *Siku Njema* , mhusika mkuu (Msanifu Kombo) hubandikwa jina la "Kongowea Mswahili" kwa kufanya bidii sana na kubombea katika lugha ya Kiswahili.

- Mama Rita anapenda kuongea sana. Hivyo basi wanakijiji wakambandika jina, Kasuku.

# Misimu

| | |
|---|---|
| **MISIMU** | |
| **Utanzu wa Fasihi** | Fasihi Simulizi |
| **Kipera cha** | Tungo Fupi |
| **Kiingereza** | Slang |

Misimu ni maneno ambayo huzuka miongoni mwa kundi fulani katika jamii na hueleweka tu miongoni mwa watu katika kundi hilo. Misimu hukua na kutoweka baada ya muda.

## Sifa za Misimu

1. Huzuka, hutumika kwa muda na hutoweka
2. Hueleweka tu baina ya kundi fulani katika jamii hasa vijana
3. Hutumia lugha fiche
4. Huchanganya ndimi

## Umuhimu wa Misimu

1. Kupitisha ujumbe
2. Kupamba lugha
3. Kutambulisha kundi husika
4. Kuburudisha

# Ushairi

| | |
|---|---|
| **USHAIRI** | |
| **Utanzu wa** | • Fasihi<br>• Nyimbo<br>• Fasihi Andishi |
| **Kiingereza** | Poetry |
| **Tutaangazia** | • Aina za Mashairi<br>• Bahari za Ushairi<br>• Uchambuzi wa Mashairi<br>• Maghani |

Ushairi ni utungo wa kisanaa unaotumia lugha teule na mpangilio fulani wa maneno badala ya kutumia lugha natharia(mflulizo).

Ushairi unaweza kuwa kipera cha fasihi simulizi (nyimbo) na pia katika fasihi andishi kwa sababu mashairi yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya kukariri na pia kwa njia ya maandishi. Mashairi yanayoghanwa badala ya kuimbwa huitwa maghani.

**Content**


- Uchambuzi
- Istilahi za Kishairi
- Sifa za Ushairi
- Umuhimu wa Mashairi


## Uchambuzi

Katika ushairi, tutaangalia:

- Aina za Mashairi - Kuainisha mashairi kulingana na idadi ya mishororo katika kila ubeti.

- Bahari za Ushairi - Muundo wa shairi kulingana vina, idadi ya mizani, vipande, mpangilio wa maneno n.k.
- Uchambuzi wa Mashairi - Mambo muhimu unayohitajika kuzingatia unapochambua shairi
- Uhuru wa Mshairi - Ukiukaji wa kanuni za sarufi
- Istilahi za Kishairi - Msamiati unaotumika katika ushairi km vina, mizani n.k
- Sifa za Ushairi - Sifa zinazobainisha ushairi kutokana na aina nyingine za sanaa.
- Umuhimu wa Ushairi - Umuhimu wa ushairi katika jamii.

# Istilahi za Kishairi

Haya ni baadhi ya maneno ambayo hautakosa kukutana nayo unapozingatia ushairi. Ni muhimu mwanafunzi kuyajua vizuri.

1. **Shairi** - ni sanaa ya maneno (utunzi maalum wa lugha ya kisanaa) unaotumia mpangilio na uteuzi maalum wa maneno na sauti ili kupitisha ujumbe fulani.
2. **Vina** - ni silabi za mwisho katika kila kipande.
3. **Mizani** - ni idadi ya silabi katika kila mshororo.
4. **Mshororo** - ni msitari mmoja wa maneno katika shairi.
5. **Ubeti** - ni kifungu cha mishororo kadhaa.
6. **Vipande** - ni visehemu vya mshororo vilivyogawanywa kwa alama ya kituo(,)
7. **Ukwapi** - kipande cha kwanza katika mshororo
8. **Mwandamo** - Kipande cha tatu katika mshororo
9. **Ukingo** - kipande cha nne katika mshororo
10. **Utao** - kipande cha pili katika mshororo
11. **Mwanzo** - mshororo wa kwanza katika ubeti
12. **Mloto** - mshororo wa pili katika ubeti
13. **Kimalizio/Kiishio** - mshororo wa mwisho katika ubeti usiorudiwarudiwa katika kila ubeti.
14. **Kibwagizo** - mshororo wa mwisho katika ubeti unaorudiwarudiwa kila ubeti.

# Sifa za Ushairi

1. Huwa na vina, mizani, mishororo na beti
2. Hutumia lugha teule
3. Hufupisha au kurefusha maneno ili kutosheleza idadi ya mizani
4. Mashairi hayazingatii kanuni za kisarufi. (Angalia uhuru wa mshairi)
5. Hutumia mbinu za lugha

# Umuhimu wa Mashairi

1. Kuburudisha
2. Kuhamasisha jamii
3. Kukuza sanaa na ukwasi wa lugha
4. Kuliwaza
5. Kuelimisha
6. Kuonya, kutahadharisha, kunasihi na kuelekeza
7. Kupitisha ujumbe fulani
8. Kusifia mtu au kitu
9. Kukejeli au kukemea mambo yanayoenda kinyume na maadili ya jamii

---

10. Mashairi yanaweza kugawanywa katika aina mbalimbali kulingana na idadi ya mishororo katika kila ubeti.
11. **Tanbihi:** Aina za Mashairi ni tofauti na Bahari za Ushairi. Aina za mashairi huzingatia idadi ya mishororo katika kila ubeti ilhali Bahari za Shairi hutegemea na muundo wa shairi kwa kuzingatia vina, mizani, vipande na mpangilio wa maneno. Shairi moja haliwezi kuwa la aina mbili (k.v tarbia na takhmisa) lakini shairi linaweza kuwa katika bahari zaidi ya moja.
12. Zifuatazo ni aina za mashairi kulingana na idadi ya mishororo katika kila ubeti

13. Aina za Mashairi

14. MISHORORO

**BAHARI ZA USHAIRI**

**Kitengo** Ushairi

AINA

| | | |
|---|---|---|
| Umoja/tathmina | 1 | Tathmina au Umoja ni shairi lenye **mshororo mmoja** katika kila ubeti. |
| Tathnia | 2 | Tathnia ni shairi lenye **mishororo miwili** katika kila ubeti. |
| Tathlitha | 3 | Tathlitha ni shairi lenye **mishororo mitatu** katika kila ubeti. |
| Tarbia | 4 | Tarbia ni shairi lenye **mishororo minne** katika kila ubeti. Mashairi mengi ni ya aina ya tarbia. |
| Takhmisa | 5 | Takhmisa ni shairi lenye **mishororo mitano** katika kila ubeti. |
| Tasdisa | 6 | Tasdisa ni shairi lenye **mishororo sita** katika kila ubeti. |
| Usaba | 7 | Usaba ni shairi lenye **mishororo saba** katika kila ubeti. |
| Ukumi | 10 | Ukumi ni shairi lenye **mishororo kumi** katika kila ubeti. |

# Bahari za Ushairi

**BAHARI ZA USHAIRI**

**Kitengo** Ushairi


**Prev** Aina za Mashairi
**Next** Uchambuzi wa Mashairi


Bahari za ushairi ni nyingi sana. Shairi huainishwa katika bahari fulani kulingana na mtindo wake, umbo lake na matumizi ya lugha.

## Mifano ya Bahari za Ushairi

1. **Utenzi** - shairi ndefu lenye kipande kimoja katika kila mshororo.
2. **Mathnawi** - ni shairi la vipande viwili (ukwapi na utao) katika kila mshororo.

   *Ewe mtunga silabi, na sauti ya kinubi,*
   *Majukumu hatubebi, maadamu hatushibi,*
   *Mateso kwa ajinabi, kwa mabwana na mabibi*
   *Ukija hayatukabi, karibia karibia*

3. **Ukawafi** - ni shairi la vipande vitatu (ukwapi, utao na mwandamo) katika kila mshororo.

   *Nashindwa nikupe nini, nishukuru kwa malezi, mapenzi na riziki,*
   *Ni pendo kiasi gani, lishindalo la mzazi, kweli mama hulipiki,*
   *Ulinilinda tumboni, ukilemewa na kazi, ila moyo huvunjiki,*
   *Kanilisha utotoni, mavazi pia malazi, ukitafuta kwa dhiki.*

4. **Mavue** - Shairi la vipande vinne (ukwapi, utao, mwandamo na ukingo) katika kila mshororo.

   *Sisi walipa ushuru, wajenga taifa, tena kwa bidii, twahangaishwa,*
   *Tumenyimwa uhuru, tuna mbaya sifa, hatujivunii, tunapopotoshwa,*
   *Kila tunapopazuru, damu na maafa, hatutulii, hali ya kutishwa*

5. **Ukaraguni** - shairi ambalo vina vyake vya kati na vya mwisho hubadilika kutoka ubetio mmoja hadi mwingine.

   *Vina Ubeti 1: ---ni, ---mi,*
   *ubeti 2: ---ta, ---lo,*
   *ubeti 3: ---po, ---wa,*

6. **Ukara** - shairi ambalo vina vya kipande kimoja havibadiliki kutoka ubeti mmoja hadi mwingine, lakini vina vya kipande kingine hubadilika. Kwa mfano, vina vya kati vinafanana kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho lakini vina vya kipande cha mwisho vinabadilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine.

   *vina Ubeti 1: ---shi, ---ma,*
   *ubeti 2: ---shi, ---ko,*
   *ubeti 3: ---shi, ---le,*
   *ubeti 4: ---shi, ---pa*

7. **Mtiririko** - shairi ambalo vina vyake vya mwisho na vya kati havibadiliki kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho.

   *kwa mfano vina vikiwa ( ---ni, ---ka) kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho.*

8. **Mkufu/pindu** - Shairi ambalo neno la mwisho au kifungu cha mwisho cha maneno katika ubeti mmoja, hutangulia katika ubeti unaofuatia.

   *Hakika tumeteleza, na njia tumepoteza,*
   *Nani wa kutuongoza, aliyepewa uweza,*
   *Filimbi akipuliza, tusiyeweza kupuuza,*
   *Bali twaisikiliza, bila ya kuzungumza,*

   *Bila ya kuzungumza, wala mwendo kulegeza,*
   *Tumwandame ja mwangaza, kututoa palipo giza,*
   *Penye dhiki ya kuliza, bila sauti kupaza*
   *Pengo hili kulijaza, ni nani anayeweza,*

9. **Kikwamba** - Neno moja au kifungu cha maneno hurudiwarudiwa kutanguliza mishororo au ubeti katika shairi.

   *Jiwe hili lala nini, ila moshi na majani,*
   *Jiwe linalala lini, litokapo vileoni,*
   *Jiwe hili halineni, lina macho halioni,*
   *Jiwe na tulibebeni, tulitupe mitaroni*

10. **Kikai** - Shairi lenye kipande kimoja kifupi (chenye mizani chache kuliko kingine) Mfano (8,4)

    *Nani binadamu yule, adumuye,*
    *Anayeishi milele, maishaye*

*Jenezani asilale, aluliye,*
*Kaburi liko mbele, sikimbiye.*

11. **Msuko** - Shairi ambalo kibwagizo/mshororo wa mwisho ni mfupi kuliko mishororo mingineyo. K.v (8,8) (8,8) (8,8) (8).

    *Hawajazawa warembo, usidhani umefika,*
    *Ukisifiwa mapambo, jinsi ulivyoumbika,*
    *Akipata jipya umbo, 'tabaki kihangaika,*
    *Usidhani umefika.*

12. **Mandhuma** - shairi ambalo kipande kimoja hutoa hoja, wazo ama swali, huku cha pili kikitoa jibu/suluhisho.
13. **Malumbano** - Mashairi mawili ambapo mshairi mmoja hutunga shairi akijibu au kupinga utunzi wa mshairi mwengine.
14. **Ngonjera** - Shairi lenye wahusika wawili wanaojibizana. K.m. Ubeti wa kwanza, mwalimu, na wa pili, mwanafunzi.
15. **Sakarani** - Shairi lenye bahari zaidi ya moja.
16. **Sabilia** - Shairi lisilokuwa na kibwagizo. Kituo (mshororo wa mwisho) hubadilika kutoka ubeti hadi ubeti.
17. **Shairi huru** - shairi lisilozingatia sheria za ushairi
18. **Shairi guni** - shairi lenye makosa ya arudhi za shairi

# Uchambuzi wa Mashairi

---

**BAHARI ZA USHAIRI**

**Kitengo** Ushairi

---

Yafuatayo ni mambo muhimu unayohitajika kuzingatia kila unapochambua shairi.

1. Muundo/Umbo la shairi
2. Uhuru wa Mshairi
3. Maudhui
4. Dhamira
5. Mtindo wa / Mbinu za Lugha

---

## Muundo/Umbo la Ushairi

Katika umbo wa shairi, tunaangazia jinsi shairi lilivyoundwa kwa kuangazia mizani, vina, mishororo n.k Aidha, ni muhimu kutaja aina na bahari za shairi zinazohusiana na kila sifa uliyoitaja.

1. **Idadi ya mishororo katika kila ubeti** - Tumia idadi ya mishororo kubainisha aina ya shairi hilo.
   Kwa mfano: *Shairi lina mishororo minne katika kile ubeti, kwa hivyo ni Tarbia*
2. **Idadi ya mizani** katika kila mshororo na katika kila kipande cha mshororo.
   Kwa mfano: *Kila mshororo una mizani kumi na sita: nane katika utao na nane katika ukwapi.*
3. **Idadi ya vipande** katika kila mshororo - Taja ikiwa shairi lina kipande kimoja, viwili, vitatu au vinne kisha utaje bahari yake.
4. **Kituo, kiishio au kibwagizo** - Ikiwa mstari wa mwisho umerudiwa rudiwa, basi shairi lina **kibwagizo** au **kiitikio**, la sivyo lina **kiishio**.
5. **Vina** - Zingatia vina vya kati na vya mwisho kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. Kisha utaje ikiwa ni **Mtiririko, Ukara au Ukaraguni**

---

## Uhuru wa Mshairi

Mshairi hafungwi na kanuni za kisarufi za lugha katika utunzi wa shairi. Anaweza kufanya makosa ya kisarufi kimakusudi ili shairi

lizingatie umbo fulani. Zifuatazo ni njia mbalimbali ambazo mtunzi wa shairi anaweza kutumia kuonyesha uhuru wake.

1. **Inkisari** - kupunguza idadi ya silabi katika neno ili kusawazisha idadi ya mizani katika mshororo.
   mfano: kubadilisha **nimeona aliyenipenda** kuwa **meona alenipenda**.
2. **Mazda** - kuongeza silabi katika neno ili kusawazisha idadi ya mizani katika mshororo.
   mfano: *afya ukijaliwa* kuwa *afiya ukijaliwa* .
3. **Tabdila** - kubadilisha silabi ya mwisho ili kustawazisha urari wa vina katika kipande bila kuathiri mizani.
   mfano: *yahuzunisha dunia* kuwa *yahuzunisha duniya* .
4. **Kuboronga Sarufi** -ni mbinu ya kupangua mpangilio wa maneno ili kuleta urari wa vina au mdundo wa ushairi.
   mfano: *siku hiyo ikifika* kuwa *ikifika hiyo siku* .
5. **Utohozi** - Kuswahilisha Maneno - Wakati mwingine mshairi anaweza kubadilisha neno la lugha nyingine litamkike kwa Kiswahili ili kudumisha mdundo wa kishairi na pia kupata neno mwafaka litakalotimiza arudhi za kiushairi.
   mfano: tukapata intaneti badala ya tukapata 'internet' ama mtandao wa tarakilishi.

---

### Maudhui

Maudhui ni jumla ya ujumbe na mawazo mbalimbali yanayojitokeza katika shairi fulani. Haya ni mambo yanayotajwa katika hadithi na yanaweza kujumuisha mawazo zaidi ya moja. Maudhui husaidia kujenga dhamira ya shairi.

---

### Dhamira

Dhamira ni lengo, dhumuni au nia ya mtunzi wa shairi. Mtunzi wa shairi anaweza kuwa na kusudi la kutuonya, kututahadharisha au kutunasihi kuhusiana na jambo fulani.

---

### Mtindo wa Lugha

Mtindo wa lugha hurejelea namna mbalimbali ambazo mshairi anatumia mbinu za lugha. Mshairi anaweza kutumia mbinu za lugha. kama vile: *Tanakali za Sauti, Istiara, Takriri, Semi n.k*

Angalia: Mbinu za Lugha katika Fasihi

# Maghani Katika Fasihi Simulizi

---

**MAGHANI**
**Kitengo** Ushairi

Maghani ni tungo zinazotolewa kwa kughanwa (nusu kuimbwa nusu kukaririwa) Maghani yanaweza kuambatanishwa na ala za muziki au kughanwa kwa mdomo tu.

## Aina za Maghani

Zipo fani mbali mbali za maghani ambazo zimeainishwa katika tanzu mbili kuu:

1. Maghani ya Kawaida
2. Maghani ya Masimulizi

### Maghani ya Masimulizi

Lengo la maghani ya aina hii ni kusimulia kisa fulani, historia, n.k.

Kuna fani mbili za Maghani ya Masimulizi:

**a) Tendi**

Tendi ni ushairi mrefu unaosimulia matukio ya kishujuaa. Tendi zinaposimuliwa huandamana na ala za muziki.

***Sifa za Tendi:***

- Ni ushairi mrefu
- Husimulia matendo ya kishujaa kwa njia kishairi
- Husimuliwa badala ya kuimbwa
- Huandamana na ala za muziki
- Husimulia visa vya kihistoria
- Hutungwa papo kwa hapo

**b) Rara**

Hizi ni hadithi fupi za kishairi zenye visa vya kusisimua, zinazosimuliwa zikiambatanishwa na ala za muziki. Aghalabu hughanwa na watoto; na hutumika kama michezo ya watoto.

***Sifa za Rara***

- Ni hadithi fupi za kishairi
- Husimulia visa vya kusisimua
- Zinaweza kuimbwa au kusimuliwa
- Huambatana na ala za muziki
- Aghalabu huwa ni visa vya kubuni

## Maghani ya Kawaida (Sifo)

Maghani ya Kawaida ni maghani yanayosifia mtu, kitu au hali katika jamii

**a) Majigambo au Kivugo**

Haya ni maghani ambayo mtunzi hujisifia (kujigamba) namna alivyo hodari katika nyanja fulani. Tungo hizi hutumia chuku na maneno ya kejeli kuwadunisha wapinzani wa mtunzi.

***Sifa za Majigambo***

- Hutumia nafsi ya kwanza
- Msimulizi hutumia maneno ya kujigamba
- Msimulizi hutumia chuku kwa wingi ili kujisifu
- Hutungwa kwa ubunifu mkubwa na hutumia mbinu kama sitiari, vidokezi, ishara n.k
- Majigambo mengi huwa mafupi, lakini baadhi yake huwa marefu.
- Huwa na matendo matukufu ya msimulizi
- Huwa na ahadi za matendo kutoka kwa msimulizi

**b) Tondozi**

Tondozi ni aina ya sifo ambayo husifia watu mashuhuri katika jamii kama vile viongozi

***Sifa za Tondozi***

- Huwa ni ushairi wa kusimuliwa
- Husifia mtu mwengine, mtu mashuhuri
- Hutumia chuku
- Hutumia mbinu kama sitiari, vidokezi, ishara n.k
- Hutaja matendo makubwa ya kiongozi anayesifiwa

**Pembezi**

Pembezi ni maghani ya kumsifu mpenzi.

***Sifa za Pembezi***

- Humsifu mpenzi wa mtu
- Aghalabu huwa ushairi mfupi
- Hutumia tamathali za lugha kwa wingi kama vile ishara kusimulia umbo la mpenzi
- Pembezi zinaweza kuandamana na ngoma

ii) Pembezi - tungo za sifa. Zinaweza kusifia kundi fulani la watu, wanyama, njaa, mvua, n.k